# UAMILIFU WA TONISHO KATIKA SENTENSI ZA KIKAMBA

**TASNIFU**

**YA**

**MUINDE, SARAH NTHENYA**

**ILIYOANDIKWA KWA MADHUMUNI YA KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI YA CHUO KIKUU CHA KENYATTA**

**2009**

Muinde,Sarah Nthenya
*Uamilifu wa tonisho katika sentensi za*
2009/333509
KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

## IKIRARI

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijawahi kutolewa kwa minajili ya kupata shahada katika Chuo Kikuu chochote.

**MUINDE, SARAH NTHENYA**

Tasnifu hii imetolewa kwa Chuo Kikuu cha Kenyatta kwa idhini yetu kama wasimamizi.

**DAKTARI ALICE NYAMBURA MWIHAKI**

**DAKTARI JACKTONE OKELLO ONYANGO**

## TABARUKU

Tasnifu hii naitoa kwa heshima ya mume wangu mpendwa Simeon Kioko aliyenitia moyo wa kufanya shahada ya uzamili.

## SHUKRANI

Kwanza kabisa namtolea Mungu shukrani kwa kuniwezesha kurudi masomoni. Kama sio Mungu nisingeweza kukamilisha kazi hii. Pia, nawashukuru wasimamizi wangu Dkt Alice Mwihaki na Dkt Jacktone Onyango walioniongoza katika kuandika kazi hii. Ahsanteni sana Mungu awabariki.

Aidha, natoa shukrani zangu kwa wahadhiri wengine wa Idara ya Kiswahili na Lugha za Kiafrika Chuo Kikuu cha Kenyatta. Namshukuru kwa dhati Bi. Gathenji aliyehakikisha kuwa nimepata vitabu vya Isimu. Mungu akubariki Bi. Gathenji na akuongezee moyo uo huo wa kusaidia. Sitasahau kushukuru Tume ya Kuwaajiri Walimu nchini kwa kunipa likizo ya kusoma. Mambo yangekuwa magumu mno bila hiyo likizo.

Aidha, nawashukuru wanafunzi wenzangu; Boniface Ngugi, Muange Willy, Andrew Nakhisa, Felicity Njurai, Hellen Ojenge na Jane Mumbua. Mlinitia moyo wa kuendelea. Nawashukuru pia wahazili wa Simecor (Machakos) walioipiga chapa kazi hii. Ahsante Bi. Lucy Kiio na Bi. Terry Mung'ala kwa kazi nzuri.

Siwezi kusahau kumshukuru mume wangu Simeon Kioko kwa kugharamia masomo yangu. Mungu akubariki na akukirimie neema yake. Mwisho nawashukuru watoto wangu Wambua, Nancy na Daniel kwa kuvumilia wakati mama yao alikuwa mwanafunzi. Mungu awaneemie msome mpate shahada za juu kuliko za mama yenu. Ahsanteni.

## UFAFANUZI WA ISTILAHI MUHIMU.

**Tonisho:** Ruwaza za kidatu katika kiwango cha sentensi sahili (kishazi).

**Toni:** Ruwaza za kidatu katika kiwango cha neno.

**Uamilifu:** Dhima ya kisarufi ambayo kwa kawaida hutofautishwa na muundo wa vijenzi.

**Maana Dhanishi:** Maana msingi ambayo pia huitwa maana tambuzi.

**Maana Tagusani:** Maana husishi ambayo kwa kawaida hutegemea na kusawiri uhusiano wa wasemaji, pamoja na uhusiano wa wasemaji na ujumbe.

**Maana Matinishi:** Maana ya kisarufi inayotegemea kanuni za kisarufi na vigezo vya umatini.

**Kishazi:** Kipashio kidogo cha kisarufi katika lugha. Baadhi ya nadharia za kisarufi hutumia kishazi kwa maana sawa na sentensi sahili.

**Kiima:** Neno ambalo hutangulia kitenzi. Uamilifu wake ni kuelekeza uhusiano wa maneno mengine kwenye sentensi.

**Yambwa tendwa:** Neno ambalo huelekezwa tendo moja kwa moja katika sentensi.

**Kijalizo:** Kiambajengo muhimu katika kishazi ambacho hukamilisha maelezo ya kitenzi.

**Shamirisho:** Sehemu ya sentensi ambayo huathiriwa na nomino na

huja baada ya kiarifu.

**Kiarifu:** Sehemu katika sentensi ambayo inaonyesha kile kinachotendwa na nomino au kiwakilishi chake.

**Chagizo:** Kipashio cha ziada na ambacho kinaweza kutolewa kwa sentensi pasi na kuathiri maana iliyokusudiwa.

**Hali:** Sehemu ya sentensi ambayo inatambulisha aina ya sentensi.

**Salio:** Sehemu inayobaki baada ya kubainisha sehemu ya hali kwenye sentensi.

**Mfanyiko:** Kitendo yakinifu au cha kiakili.

**Kirai:** Kifungu cha maneno ambacho huwa ni sehemu ya sentensi na huwa ni kipashio cha kimuundo chenye neno moja au zaidi.

**Shamirisho:** Kategoria ya maneno ambayo inatumiwa kuanzisha vishazi tegemezi.

**Maudhui:** Kiambajengo muhimu katika kishazi ambacho hubeba nomino na viwakilishi vyake kwenye mtazamo wa kishazi kama ujumbe.

## MAANA YA VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| S.A.M: | Sarufi Amilifu Mfumo |
| KP: | Kirai Patanishi |
| P: | Kipatanishi |
| KN: | Kirai Nomino |
| N: | Nomino |
| KT: | Kirai Tenzi |
| T: | Kitenzi |
| KE: | Kirai Elezi |
| E: | Kielezi |
| KV: | Kirai Vumishi |
| V: | Kivumishi |
| KH: | Kirai Husishi |
| H: | Kihusishi |
| KSH: | Kirai Shamirishi |
| SH: | Shamirishi |
| KB: | Kirai Kibainishi |
| B: | Kibainishi |
| S: | Sentensi |
| K: | Kiima |
| Ki: | Kiarifa |
| SH: | Shamirisho |

# IKISIRI

Utafiti huu ulitekelezwa kwa madhumuni ya kuchambua na kujadili ruwaza za tonisho katika sentensi za Kikamba, ili kubainisha muundo na uamilifu katika nyanja za sintaksia na pragmatiki. Uchanganuzi ulitegemea mihimili ya Sarufi Amilifu Mfumo, hasa amali za lugha, tanzu za kisarufi na mitazamo ya kishazi. Nadharia ya Sarufi Amilifu Mfumo ilishirikisha misingi ya kimuundo ya Sarufi Zalishi. Swala la utafiti lilikuwa kudhihirisha uamilifu wa tonisho katika sentensi za Kikamba kupitia dhima za kisintaksia na kipragmatiki. Mbinu za utafiti zilijumuisha nyanjani na maktabani. Matokeo ya utafiti yaliwakilishwa kwa njia ya maelezo katika sura nne.

Sura ya kwanza ilichambua usuli wa mada na kubainisha suala la utafiti, malengo na tahakiki za utafiti, misingi ya kuchagua mada, tahakiki ya maandishi, misingi ya kinadharia na mbinu za utafiti. Sura ya pili ilifafanua muundo wa sentensi za Kikamba. Dhima kuu ya sura hii ilikuwa kutambulisha maneno na kuchanganua miundo virai vyake, kwa madhumuni ya kuwakilisha sentensi za Kikamba. Uchanganuzi wa kishazi ulifanywa kupitia mitazamo mitatu ya kishazi. Ruwaza za tonisho katika hivi vishazi zilibainishwa kwa mujibu wa maana na uamilifu wake katika sura ya tatu. Tonisho ni kigezo muhimu katika sarufi ya Kikamba na ina mchango katika uwanja wa sintaksia kwa jumla pamoja na utumikizi katika ufundishaji wa lugha.

## YALIYOMO


| Mada | Ukurasa |
|---|---|
| Ikirari | ii |
| Tabaruku | iii |
| Shukrani | iv |
| Ufafanuzi wa Istilahi Muhimu | v |
| Maana ya Vifupisho | vii |
| Ikisiri | viii |
| **Sura ya Kwanza: Utangulizi** | 1 |
| 1.1.0 Suala la Utafiti | 4 |
| 1.2.0 Malengo ya Utafiti | 4 |
| 1.3.0 Maswali ya Utafiti | 5 |
| 1.4.0 Tahadhania za Utafiti | 5 |
| 1.5.0 Upeo na Mipaka ya Utafiti | 6 |
| 1.6.0 Misingi ya Kuchagua Mada ya Utafiti | 7 |
| 1.7.0 Tahakiki za Maandishi | 8 |
| 1.7.1 Maandishi ya Kijumla kuhusu Tonisho | 8 |
| 1.7.2 Maandishi ya Kibantu kuhusu Tonisho | 10 |
| 1.7.3 Tafiti Bayana za Tonisho katika Lugha za Kibantu | 11 |
| 1.8.0 Misingi ya Kinadharia | 13 |

1.8.1 Mihimili ya Sarufi Amilifu Mfumo 14

1.8.2 Mitazamo ya Kishazi 17

1.9.0 Mbinu za Utafiti 21

1.9.1 Mbinu za Kukusanya Data 22

1.9.2 Mbinu za Kuchanganua Data 24

1.9.3 Mbinu za Kuwasilisha Data 24

**Sura ya Pili: Muundo wa Sentensi za Kikamba** 26

2.1.0 Kategoria na Dhima za Maneno 26

2.1.1 Nomino 28

2.1.2. Vitenzi 32

2.1.3 Vivumishi 36

2.1.4 Vielezi 38

2.1.5 Vihusishi 39

2.1.6 Vibainishi 40

2.1.7 Shamirishi 42

2.1.8 Vipatanishi 43

2.2.0 Miundo Virai 44

2.2.1 Kirai Nomino 47

2.2.2 Kirai Tenzi 49

2.2.3 Kirai Vumishi 51

2.2.4 Kirai Elezi 52

2.2.5 Kirai Husishi 54

2.2.6 Kirai Bainishi 55

2.2.7 Kirai Shamirishi 57

2.2.8 Kirai Patanishi 59

2.3.0 Uamilifu wa Vishazi 63

2.3.1 Kishazi kama Ujumbe 65

2.3.2 Kishazi kama Upokezano 68

2.3.0 Kishazi kama Uwakilishi 72

**Sura ya Tatu : Ruwaza Tonisho katika Kikamba** 82

3.1.0 Tonisho Sintaksia 82

3.1.1 Tonisho katika Sentensi Arifu 83

3.1.2 Tonisho katika Sentensi Ulizi 84

3.1.3 Tonisho katika Sentensi Yakinishi 89

3.1.4 Tonisho katika Sentensi Kanushi 91

3.2.0 Tonisho Pragmatiki 94

3.2.1 Tonisho katika Sentensi zenye Dhamira Amrifu 94

3.2.2 Tonisho katika Sentensi zenye Dhamira ya Mshangao 96

3.2.3 Tonisho katika Sentensi zenye Dhamira ya Huzuni 98

3.2.4 Tonisho katika Sentensi zenye Dhamira ya Kusihi 99

3.2.5 Tonisho katika Sentensi za Kejeli 101

3.2.6 Tonisho katika Sentensi zenye Hasira 103

3.2.7 Tonisho katika Sentensi zenye Msisimko 105

3.2.8 Tonisho katika Sentensi zenye Uoga 106

3.2.9 Tonisho katika Sentensi zenye Ukakamavu 108

**Sura ya Nne: Hitimisho** 113

4.1.0 Matokeo ya Utafiti 115

4.2.0 Mahitimisho ya Utafiti 119

4.3.0 Mapendekezo Zaidi ya Utafiti 121

Marejeleo 122

Kiambatisho 128

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

**Usuli wa Mada.**

Lugha hutumika kwa kiamilifu kulingana na mahitaji ya wanaoisema. Kunayo lugha zungumzwa na lugha ya maandishi. Aina zote mbili ni muhimu katika kutekeleza mawasiliano (Halliday 1985). Ili kutekeleza mawasiliano kamili, lugha iliyoandikwa hutumia uakifishaji ambao unaweka mipaka baina ya vitengo tofauti vya kisarufi. Lugha-zungumzwa nayo inatumia sifa ya tonisho ili kuweka hiyo mipaka pamoja na kupasha ujumbe kamili. Katika utafiti huu, tuliangaza uamilifu wa tonisho.

Mada ya tonisho inashughulikiwa kimsingi katika usomi wa kisarufi. Kwa kutumia tonisho, wanasarufi wana uwezo wa kuainisha lugha zungumzwa na kuipanga katika vipengele vya kisarufi kwa mujibu wa umuhimu wake katika mawasiliano (Halliday 2004). Baadhi ya vipengele hivi ndivyo tulivyochunguza kwenye utafiti huu wenye mwelekeo wa uwanja wa Sarufi Amilifu. Tuliangaza utanzu wa tonisho sintaksia na tonisho pragmatiki.

Tonisho sintaksia ina uamilifu wa kudhihirisha matumizi ya dhima tofauti katika sentensi. Mipaka ya kisarufi kwenye vishazi hufafanuliwa kwa tonisho (Williams 1973 na William 1992). Aidha tonisho sintaksia hubainisha aina za sentensi kama vile sentensi swalifu na arifu, sentensi kanushi na yakinifu (Matthews 1981,

Crystal 1985, Cruttenden 1986, Crystal 1987, Bolinger 1989, Malmkjær 1991). Ruwaza za tonisho hutawaliwa na kanuni maalum kulingana na sentensi husika. Hivyo basi, tonisho ina dhima ya kisintaksia ya kuipa sentensi sura ya kisarufi na pia kupasha ujumbe kamili.

Kwa upande wa tonisho pragmatiki, dhamira za wasemaji hudhihirika. Pragmatiki inahusu mambo yasiyosemeka kama vile furaha, mshangao, uoga, kusihi, huzuni na mengine mengi ambayo hutambulika kwa matumizi ya tonisho. Katika kiwango hiki, tonisho hutumika pamoja na sifa zingine za kiarudhi kama vile mkazo na lugha-ishara ili kutoa mawasiliano kamili (Bolinger 1968 na Crystal 1987). Kauli hii ina maana kuwa mawasiliano yanahusu sio tu yaliyosemwa bali vile yalivyosemwa. Hivyo basi, tonisho pragmatiki inadhihirisha maana na matumizi ya lugha kwa mujibu wa msemaji, msikilizaji na muktadha wa ule usemi (Levinson 1993, Richards, Weber & Platt 1985, Finch 2000). Katika kipengele hiki vilevile tonisho pragmatiki hutumiwa kudhihirisha lugha adabu.

Uchaguzi wa maneno katika lugha adabu unategemea uhusiano wa mtu na wengine na uamilifu wa vipengele vya kiisimu ambavyo amevichagua. Tonisho huenda ikatumika kudhihirisha ukosefu wa adabu ama ikaonyesha adabu. Hivyo basi tonisho pragmatiki hufafanua maana kamili ya usemi na pia hufanikisha mawasiliano. Mawasiliano ni jambo la kimsingi mno na ambapo lugha inatumika, lazima kuwe na hali ya kuchagua ni vipengele vipi vya kutumia. Kwa mujibu wa



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

ukweli huu, tonisho inatumika katika lugha zungumzwa ili kukidhi mahitaji ya mawasiliano. Utafiti huu umechanganua sentensi za Kikamba.

Kikamba ni lugha ya toni inayobainisha maana-leksika ( Ford 1975, Mutiga 2002 & Kioko 2005). Lugha toni ni lugha itumiayo kidatu kubainisha maana za kileksia. Aidha, Kikamba ni lugha ya Kibantu ambayo inatumiwa katika Mkoa wa Mashariki. Guthrie (1967) aliiorodhesha lugha hii 'E35' (E ni herufi inayosimamia Mashariki katika Kiingereza) ambayo ni Kanda la Bantu la Mashariki.

Kama familia ya lugha za Kibantu, Kikamba kina vigezo vifuatavyo vya Ubantu. Kwanza, msamiati wake wa kiasili unakurubiana na lugha zingine za Kibantu. Kimofolojia, maumbo ya maneno ya Kikamba ni kama ya lugha zingine za Kibantu. Maumbo ya maneno yanafuata utaratibu wa kuambishwa viambishi. Aidha, mfumo wa sauti katika lugha hii unadhihirisha Ubantu kwa kuwa silabi zake zote ni wazi. Hakuna silabi funge yaani silabi inayoishia kwa konsonanti. Vilevile, mpangilio wa maneno kwenye ngeli umefuata utaratibu wa lugha zingine za Kibantu. Ingawa kigezo kingine cha Ubantu ni kuhusisha toni bainifu, utafiti huu uliepusha toni na kushughulikia tonisho ambayo inadhihirika katika kiwango cha sentensi.

### 1.1.0 Suala la Utafiti.

Utafiti huu ulidhamiria kuchanganua na kujadili ruwaza za tonisho katika sentensi za Kikamba kwa madhumuni ya kufafanua muundo na kudhihirisha uamilifu wake. Kwa jumla, ufafanuzi huu ulijikita katika dhima za sintaksia na pragmatiki. Kipashio cha kisarufi ambacho kilichanganuliwa ni kishazi au kwa maneno mengine sentensi sahili.

Kuna tafiti zilizofanywa kuhusu tonisho (K.m Ford 1975) ambazo zilichunguza toni kwenye maneno na sentensi sahili. Kando na kuwa zinadhihirisha uamilifu wa kisemantiki, tafiti hizi zimepungukiwa kisintaksia na kipragmatiki kwa sababu zinadhihirisha tu tonisho fonolojia. Tonisho sintaksia na tonisho pragmatiki ni muhimu kwa sarufi ya Kikamba kwa sababu ya uamilifu wake wa kufafanua aina za sentensi na dhamira zake mtawalia. Hivyo basi kuna haja ya kutafiti juu ya tonisho sintaksia na tonisho pragmatiki na hasa kwa mtazamo wa nadharia za kisasa. Utafiti huu una nafasi ya kuchangia katika nadharia za kiisimu, hasa kwa misingi ya Sarufi Amilifu, na pia kupanua maarifa kuhusu sarufi ya tonisho katika Kikamba.

### 1.2.0 Malengo ya Utafiti.

1. Kuainisha vijenzi tofauti vya sentensi za Kikamba na kuonyesha uamilifu wake wa kisarufi.

2. Kuchanganua ruwaza za tonisho katika sentensi za Kikamba.
3. Kutathmini uamilifu wa tonisho katika sentensi za Kikamba kwa kuzingatia dhima za kisintaksia na kipragmatiki.
4. Kuchanganua kanuni za tonisho sintaksia na tonisho pragmatiki kwa kurejelea nadharia ya Sarufi Amilifu Mfumo.

## 1.3.0 Maswali ya Utafiti.

1. Vijenzi vya sentensi za Kikamba huainishwa namna gani na huwa na uamilifu gani wa kisarufi?
2. Ruwaza za tonisho katika sentensi za Kikamba huchukua mipangilio gani?
3. Uamilifu wa tonisho katika sentensi za Kikamba ni upi ambapo dhima za kisintaksia na kipragmatiki zimezingatiwa?
4. Kanuni za tonisho sintaksia na tonisho pragmatiki zinahusiana vipi na nadharia ya Sarufi Amilifu Mfumo?

## 1.4.0 Tahadhania za Utafiti.

1. Sentensi za Kikamba zinadhihirisha uamilifu wa tonisho kisintaksia na tonisho kipragmatiki kwa mujibu wa Isimu Amilifu.
2. Ruwaza za tonisho katika sentensi za Kikamba ni bayana na huchangia katika sarufi ya Kikamba.

### 1.5.0 Upeo na Mipaka ya Utafiti.

Baadhi ya wasomi (k.m Bolinger 1968, Williams 1973, Crystal 1985, 1987, Ladd 1996 na Brazil 1980), wanasema kuwa tonisho hudhihirika kwa mitazamo tofauti. Mtazamo mmoja ni wa kifonolojia. Tonisho kifonolojia hudhihirika wakati sauti za usemi zinasikika kwa mfululizo ambao unabadilikabadilika kama vile mawimbi ya kiakustika. Yale maumbo ya fonolojia yanafuata mkondo wa kidatu unaounganisha vile vigezo vya sauti katika usemi. Tuliepusha mtazamo huu wa tonisho kifonolojia kwa sababu unashughulikia hasa kudhihirisha zile taratibu za utoaji wa sauti. Hata hivyo, mtazamo huu ulichangia kwa utafiti huu pale ambapo tulitaka kudhihirisha ni wapi kidatu kimepanda au kushuka katika kukidhi dhima za kisintaksia au dhima za kipragmatiki.

Mtazamo wa pili ni tonisho sintaksia. Tonisho sintaksia hupasha maana katika kiwango cha kishazi (Ladd Ibid). Mtazamo huu hauzingatii sifa kama vile mkazo, kiinitoni, na toni, ambazo hudhihirika katika kiwango cha neno na ambazo hutofautisha maana ya kimsingi ya maneno. Tonisho sintaksia hutofautisha hali za sentensi kimatamshi. Mtazamo wa tatu ni wa tonisho pragmatiki ambayo inahusu dhamira za msemaji.

Vilevile kuna tonisho isimujamii (Crystal 1985 na Richards, Weber & Platt 1985). Waandishi hawa wanasema kuwa tonisho inaweza kutambulisha asili ya mtu. Jambo hili hudhihirika pale ambapo ruwaza za tonisho huweza kutofautiana baina

ya lugha moja na nyingine na pia lugha moja inaweza kuwa na ruwaza tofauti za tonisho kwa mujibu wa mahali inapotumika (Bolinger 1989). Tonisho isimujamii pia inatofautisha umri wa wanenaji na pia jinsia zao. Ruwaza za tonisho zinazodhihirika wazee wanapoongea ni tofauti na za vijana. Aidha wanawake na wanaume hutofautiana kwa mujibu wa ruwaza za tonisho zinazodhihirika wanapoongea. Tuliepusha tonisho isimujamii kwa sababu haihusiki moja kwa moja na mambo ya kisarufi. Huu ni utafiti wa isimu na hasa sarufi ya tonisho kwa hivyo tonisho katika isimujamii haikuchangia.

Katika utafiti huu, tulishughulikia mada mbili tu ambazo ni tonisho sintaksia na tonisho pragmatiki. Ruwaza tofauti za tonisho kwenye kanuni hizi mbili zilibainishwa na kufafanuliwa kwa kutumia sentensi sahili. Tonisho fonolojia haikushughulikiwa na ingefaa pia kwa mchango wa kimsingi wa kazi ya kisintaksia.

### 1.6.0 Misingi ya Kuchagua Mada ya Utafiti.

Mada hii ilichaguliwa kwa madhumuni ya mchango wake katika Isimu. Kwa upande wa kisintaksia, hali tofauti za sentensi na vijenzi vyake zilidhihirishwa. Mikondo tofauti ya ruwaza za tonisho ilibainishwa. Kwa hivyo tonisho sintaksia iliainisha aina tofauti za sentensi. Katika hali hii pia utafiti huu ulikusudia kupata nafasi ya kuchangia katika ufafanuzi wa sarufi ya Kikamba.

Kwa upande wa tonisho pragmatiki, dhamira tofauti zilizodhihirishwa na tonisho zilifafanua maana tofauti za sentensi. Dhamira hizi zilidhihirisha matumizi tofauti ya sarufi ya Kikamba na uamilifu wake katika mawasiliano. Tonisho pragmatiki katika Kikamba ina mchango wa kufafanua yaliyosemwa na sentensi. Aidha, tonisho pragmatiki inachangia kwa sarufi ya Kikamba.

Kwa upande wa utumikizi, matokeo ya utafiti huu yanaweza kusaidia katika ufundishaji wa lugha ya Kikamba na hasa ambapo lugha yenyewe inatumika katika kufundishia. Ufundishaji katika lugha hii, kando na kuangazia vipengele vya kisarufi vya kuandika, utajumuisha pia tonisho na uamilifu wake katika sarufi. Aidha, sentensi sahili zilizokusanywa kama data zinaweza kutumika katika kufanya utafiti zaidi katika lugha hii ya Kikamba. Hebu tufafanue tahakiki ya maandishi.

**1.7.0 Tahakiki ya Maandishi.**

Tulichambua maandishi jumuifu kuhusu tonisho, kisha maandishi ya kijumla kuhusu tonisho ya Kikamba na lugha zingine za Kibantu. Hatimaye tuliangaza tafiti bayana za tonisho katika Kibantu pamoja na Kikamba.

**1.7.1 Maandishi ya Kijumla kuhusu Tonisho.**

Baadhi ya waandishi (k.m Martinet 1962, Bolinger 1968, Maw 1969, Crystal 1985, Cruttenden 1986, Bolinger 1989 na Kimble-Fry 2001) wanasema kwamba

tonisho huwa na uamilifu wa kupasha ujumbe wa ziada kando na kutumika kama uakifishaji kwenye lugha zungumzwa. Aidha, tonisho inatumika katika kubadilisha mada ambapo kidatu cha juu hutumika kuanzisha mada na kidatu cha chini kinadhihirisha kukamilika kwake. Kwa hivyo, tunaweza kusema kuwa, tonisho hudhihirisha uamilifu wa kiusemi ambapo hali tofauti za sentensi zinabainika pamoja na dhamira za wazungumzaji.

Tonisho imetambuliwa na wanaisimu sio tu katika kubainisha mipaka ya kisintaksia bali pia kutoa maana kwa usemi (Taz. Pike 1946, Guthrie 1948, Halliday 1970, Bolinger 1972, Williams 1973, Matthews 1981, Mamkjær 1991 na Finch 2000). Sentensi moja inaweza kuwa na maana tofauti kulingana na ruwaza tofauti zilizotumika. Vilevile, tonisho inapotumika sio rahisi kuweka bayana tofauti baina ya maana kisintaksia na dhamira ya mzungumzaji. Dhamira ya mzungumzaji pia huwa na maana katika usemi. Kwa hivyo, tunaweza kusema kuwa tonisho hudhihirisha uamilifu wa kiusemi ambapo hali tofauti za sentensi zinabainika pamoja na dhamira za wazungumzaji.

Wanaisimu wengine (k.m Halliday 1985, 2004 na Crystal 1987) wanahusisha tonisho na 'umbo la taarifa'. Wanasema kuwa tonisho ni njia inayotumiwa na msemaji kubainisha taarifa mpya na inayojulikana tayari. Halliday (2004) pia amefafanua tonisho kama inayotumika kwa kile alichokiita 'kando ya kishazi'. Hii

ina maana kuwa, kando na mpangilio wa kishazi, kuna matumizi ya tonisho na wizani ambazo ni sifa za kukamilisha maana katika usemi.

Tonisho, ni sifa halisi inayotumiwa na kila lugha katika kukamilisha mawasiliano. Kuchagua na kutumia ruwaza fulani ya tonisho ni jambo la kiasili na la kawaida kwa msemaji kutegemea ujumbe anaodhamiria kuupasha. Aidha, tonisho hukamilisha ujumbe zaidi ambapo lugha ishara inatumika. Lugha ishara inahusu matumizi ya viungo vya mwili kama vile mikono, kichwa na uso; ishara zinazoenda sambamba na usemi ambapo msemaji anaongea. Ishara hizi pamoja na tonisho huchangia katika mawasiliano.

Kwa mwenyeji wa lugha, tonisho humudiwa kama sarufi yoyote ile. Watoto hujifunza na kudhibiti tonisho kadri wanavyokua na kujifunza ile lugha huku wakiihusisha na tajriba zao za maisha. Hivyo basi, tonisho kama vipengele vingine vya sarufi, hubidi kutiliwa maanani na kuzingatiwa ili itumike vizuri na kuleta maana iliyokusudiwa. Maelezo haya yamechambua maandishi kwa jumla lakini yanaweza pia kuangaza kanuni za aila ya lugha kama vile Kibantu.

### 1.7.2 Maandishi ya Kibantu Kuhusu Tonisho.

Sehemu hii inahakiki maandishi ya Kibantu kuhusu tonisho. Tahakiki hii imeangaza waandishi kadha na kuchambua yale wamesema kuhusu tonisho kwenye lugha kadha za Kibantu zikiwemo: Kiswahili, Lingala na Kikuyu.

Lugha za Lingala, Kiswahili na Kikuyu zimebainisha ruwaza kadha za tonisho (Taz. Ashton 1944, Guthrie 1948, Armstrong 1967, Maw 1969, Mohammed 2001, Habwe na Karanja 2004). Katika sentensi za kuarifu, za amri za maombi na za maswali ya maelezo, ruwaza za tonisho hushuka mwishoni mwa sentensi. Sentensi za maswali yanayotarajiwa kujibiwa 'ndiyo' au 'la' hutumia ruwaza tofauti. Kidatu huanza kupanda katika silabi ya kati na hupanda zaidi katika silabi ya pili kutoka mwisho katika neno la mwisho katika sentensi.

Maelezo haya yanadhihirisha ukuruba uliopo katika matumizi ya tonisho katika lugha za Kibantu. Tofauti inayojitokeza ni pale ambapo lugha moja inapandisha au kushusha ile tonisho zaidi ya lugha nyingine. Madai haya yalihakikiwa zaidi kuhusiana na tafiti bayana za tonisho katika lugha za Kibantu.

### 1.7.3 Tafiti Bayana za Tonisho katika Lugha za Kibantu.

Sehemu hii imeangaza tafiti tatu ambazo zimeshughulikia tonisho katika lugha za Kibantu. Lugha ambazo tumeshughulikia ni Dzamba, Likila, Lingala, Kikuyu na Kikamba. Watafiti husika ni wawili: Ford (1974, 1975) na Bokamba (1976).

Bokamba (Ibid) alitafiti juu ya lugha tatu za Kibantu ambazo ni Dzamba, Likila na Lingala. Katika lugha hizi, alichunguza maendelezo ya sentensi za maswali kisintaksia na kisemantiki. Mahitimisho na matokeo ya utafiti wake ni kwamba,

katika lugha hizi za Kibantu, maswali yanayotarajiwa kujibiwa 'ndiyo' au 'la', yanategemea tonisho peke yake ili kuweza kueleweka.

Bokamba (Ibid) anasema kwamba, katika sentensi za kuarifu, tonisho huanza kwa kushuka halafu inapanda katikati mwa sentensi kisha inashuka mwishoni mwa sentensi. Kushuka kunakodhihirika mwishoni mwa sentensi huwa kwa chini zaidi kuliko mwanzoni. Nayo maswali yanayohitaji majibu ya 'ndiyo' au 'la' huanza kwa kidatu cha juu zaidi kuliko sentensi za kuarifu na kupanda zaidi mwishoni. Alitumia nadharia ya Sarufi-Geuza maumbo Zalishi.

Ford (1974) alifanya utafiti juu ya toni na tonisho katika lugha ya Kikuyu. Mtafiti huyu alichunguza matumizi ya tonisho katika kutofautisha hali tofauti za sentensi. Kwenye utafiti huu, Ford alishughulikia mfumo wa toni unaobainisha fonimu za toni na mwingiliano wake. Matokeo na mahitimisho yake ni kuwa matumizi ya tonisho hubainisha hali tofauti za sentensi kama vile taarifa, amri na aina za maswali. Alitumia nadharia ya Sarufi Geuza – maumbo Zalishi.

Aidha Ford (1975) alifanya utafiti kuhusu toni na tonisho katika Kikamba. Kwenye utafiti huu ambao aliufanya Kangundo, Wilaya ya Machakos, Ford (Ibid) alichunguza toni katika nomino na vitenzi. Kwa upande wa tonisho, alitumia alama za toni kuonyesha ruwaza za tonisho jambo linalotufanya tukisie kuwa utafiti wake ulihusu tonisho kifonolojia. Kielelezo cha kazi yake ni kama hiki:



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

*ndò:tò ndò:ku* 'ndoto mbaya'. Aidha alitumia nadharia ya Sarufi Geuza-maumbo Zalishi. Tonisho fonolojia haikugusiwa katika utafiti wetu isipokuwa pale ilipoangaza kueleweka kwa utafiti huu.

Hata hivyo, Ford (1975) amebainisha kuwa sentensi taarifa za kinyume, sentensi za amri za kinyume na sentensi yakinishi, hutumia tonisho tofauti zikilinganishwa na sentensi taarifa yakinishi. Aidha, maswali ya moja kwa moja (yasiyotumia viulizi), hutumia tonisho ya juu kuliko sentensi za taarifa na amri. Tofauti iliopo ni kuwa ametumia toni kueleza na kudhihirisha hizi tofauti. Vilevile hakutumia michoro ya ruwaza za tonisho kama ilivyo kwenye utafiti huu. Michoro ya ruwaza za tonisho husaidia kudhihirisha kwa uwazi na kwa uwekevu zaidi mikondo inayofuatwa na hizi sentensi.

Hivyo basi, kulingana na tahakiki yetu, tafiti hizi zimejiunga na utafiti wetu isipokuwa kwa mambo mawili. Kwanza, utafiti wetu umechunguza tonisho sintaksia na tonisho pragmatiki katika kiwango cha sentensi. Pili, tumetumia nadharia tofauti ambayo ni Sarufi Amilifu Mfumo.

### 1.8.0 Misingi ya Kinadharia.

Nadharia inayofaa kwa utafiti huu ni Sarufi Amilifu (Taz. Halliday 2004). Sarufi Amilifu ina mitazamo miwili ya kijumla; Sarufi Amilifu Leksia na Sarufi Amilifu Mfumo. Utafiti huu ulitegemea mihimili ya Sarufi Amilifu Mfumo (SAM).

Mihimili husika inazingatia lugha kama mfumo wa maana na mitazano mitatu ya kishazi.

### 1.8.1 Mihimili ya Sarufi Amilifu Mfumo.

Sarufi Amilifu Mfumo (SAM) inaeleza jinsi ambavyo lugha inatumika katika hali halisi ya mawasiliano. Kimsingi, SAM hurejelea lugha kama mtandaa wa maana na uamilifu wa vipengele vinavyoihusu na kubainisha aina tatu za maana: maana dhanishi, maana tagusani, na maana matinishi.

Maana dhanishi kwa jina lingine ni maana tambuzi. Amali hii ni kitengo cha maana ambacho kinawakilisha uwezo wa msemaji wa kutambua mambo. Maana dhanishi ndiyo hubeba maudhui katika lugha. Kupitia maana dhanishi, tajriba za watu huwakilishwa. Tajriba hizi ni za ulimwengu wa kitamaduni na kijamii, tunamoishi na ule wa mtu binafsi. Maana dhanishi inatuwezesha kutwaa ujuzi wa ulimwengu tunamoishi na pia tajriba zetu.

Maana dhanishi inawakilisha utanzu wa kisarufi wa semantiki. Semantiki inashughulika kijumla, mfumo wa maana katika lugha kama unavyoelezwa na sarufi na msamiati wa ile lugha. Lugha hujenga mambo ya kisemantiki ambayo yanatuwezesha kufikiria kuhusu tajriba zetu. Kauli hii ina maana kwamba, semantiki ndiyo inafasiri na kutwaa maana katika tajriba zetu. Maana dhanishi haikamiliki bila maana tagusani.

Maana tagusani ni maana husishi. Inasimamia kitengo tangamanishi cha matumizi ya lugha kutegemea vikwazo vya kimawasiliano katika jamii. Maana tagusani inawafaa wasemaji wa lugha kama nyenzo ya kufasili na kutafsiri wajibu wa dhima ya kijamii (Kihara 2006). Kupitia maana tagusani wasemaji wanatumia lugha kwa minajili ya kuasisi, kuimarisha na kudumisha masharti ya mahusiano ya kijamii.

Maana tagusani inabainika kama amali tekelezi ya lugha. Amali tekelezi inazingatia matumizi ya lugha kama tendo la usemi. Msemaji ni mtenda, ambaye hujiingiza katika tendo hilo. Hivi ni kusema kwamba, msemaji ni mshirika wa tendo la usemi, kwa namna ambavyo anajiingiza katika mkutadha na hali halisi ya mawasiliano ili aweze kujieleza na kueleweka. Msemaji anaeleweka kwa kugusia mielekeo, imani, tabia, falsafa, hisia na mawazo ya msikilizaji. Kwa hivyo, maana tagusani inatazama kaida za vikwazo jumulifu vya kimawasiliano katika jamii.

Kwa upande wa kisarufi, maana tagusani inaoana na utanzu wa pragmatiki. Lugha ni ishara ya kipragmatiki. Pragmatiki huangalia lugha kama mfumo wa maana kwa kutegemea muktadha wa mawasiliano. Kwa hivyo, pragmatiki ni utanzu wa kisarufi ambao hauwezi kupuuzwa kama mawasiliano yataeleweka. Mawasiliano yatakamilika tu pale ambapo pragmatiki itafafanua kile ambacho msemaji anaweza kumaanisha mbali na kile asemacho kwa uwazi.

Kwa pamoja, maana dhanishi na maana tagusani huwakilisha amali kuu za lugha. Amali hizi kuu hutimiza makusudio mawili makubwa ya lugha ambayo ni ya kuelewa mazingira na kuingiliana na wengine kwenye yale mazingira mahsusi. Hata hivyo, maana tagusani, sawa na maana dhanishi, hupata uyakinifu wake kupitia maana matinishi.

Maana matinishi inarejelea jumla ya kanuni za sarufi na ufasaha wa matumizi ya lugha. Hivi ni kusema kwamba maana matinishi inaelekeza matumizi ili kumpatia msemaji vifaa vya kuwasilisha ujumbe kwa njia yenye usarifu na ufasaha kulingana na vikwazo vya muktadha na hali ya mawasiliano. Kwa misingi ya kisarufi tunafunganisha maana matinishi na utanzu wa sintaksia. Sintaksia inahusika na kanuni za mpangilio wa maneno katika sentensi na sheria zinazoambatana na mpangilio huo (Taz. Richards, Platt na Weber 1985 na Radford 1997). Ni lazima ule mpangilio na uhusiano wa maneno kwenye sentensi au matini uwe na maana. Ukweli huu ndio unatuwezesha kusema kwamba, sintaksia hudhibitiwa na semantiki.

Kwa jumla, maana matinishi (ambayo inawakilisha matini), huweza kuwasilisha ujumbe namna ulivyodhamiriwa kupitia kwa ushirikiano wa maana dhanishi kwa upande mmoja, na maana tagusani kwa upande mwingine. Uwasilishi na uchanganuzi wa matini unarejelea mitazamo mbalimbali ya kishazi.

### 1.8.2 Mitazamo ya Kishazi.

Matini ndogo ya kisarufi ambayo hutumiwa kama msingi wa uchanganuzi katika SAM ni kishazi. Kishazi kimetambuliwa kuwa kipashio kidogo katika sarufi ambacho kinaweza kuchanganuliwa katika muktadha wa mawasiliano (Crystal 1985 na Radford 1997). Halliday (1985) amezungumzia mitazamo mitatu ya kishazi: kishazi kama uwakilishi, kishazi kama upokezano, na kishazi kama ujumbe.

Kishazi kama ujumbe ni sifa ya lugha zote. Aghalabu, lugha nyingi hupanga kishazi kama ujumbe kikitanguliwa na sehemu ya maudhui kisha kijalizo. Kauli hii inaweza kuwakilishwa katika Kikamba kama ifuatavyo.

**(1.1) Kielelezo cha Kishazi kama Ujumbe.**

| Maudhui | Kijalizo |
|---|---|
| *Malia*<br>'Maria | *nĩwathi ndũnyũ.*<br>ameenda sokoni' |
| *We*<br>'Yeye | *nĩ mũseo.*<br>ni mzuri.' |
| *Athaũki onthe*<br>'Wachezaji wote | *nĩ mokie.*<br>Wamekuja'. |

Kishazi kama ujumbe pia huwakilisha maudhui na hali katika sarufi. Kila kishazi huru huwa kinachagua hali fulani. Hali yenyewe inaweza kuwa taarifa au swali. Maswali yanaweza kuwa yenye viswalishi au yanayotarajia majibu ya 'ndiyo' au 'la'. Katika Kikamba, mpangilio wa maneno katika sentensi za taarifa na sentensi za maswali ya 'ndiyo /la' huwa hazibainiki tofauti kimaana bila matumizi ya tonisho. Hivyo basi hali ya sentensi inafafanuliwa kwa matumizi ya tonisho. Kishazi kama ujumbe ni mhimili ambao ulitumiwa kutathmini maana na dhana zilizotumiwa katika sentensi tofauti. Kila mpangilio wa sentensi unapaswa kuwa na ujumbe wenye maana na pia umantiki. Hebu tufafanue kishazi kama upokezano.

Kishazi kama upokezano huwa kimepangwa kama tukio la mtagusano kati ya msemaji na hadhira yake. Katika kitendo cha kuongea, msemaji hujitwika jukumu la kiusemi na katika hali hiyo hiyo anampokeza msikilizaji jukumu lake vilevile. Kwa mfano, msemaji anapouliza swali, bila shaka anatarajia jibu kutoka kwa msikilizaji. Aidha, msemaji anapomwamrisha msikilizaji, anamtarajia msikilizaji atii amri yake. Hivyo basi, katika kishazi kama upokezano, ama msemaji anampa kitu msikilizaji au anataka kitu kutoka kwake. Yale yanayopokezanwa ni bidhaa na huduma ama taarifa. Mambo haya yakiainishwa yanaweza kuwekwa kwa vifungu vinne vya kimsingi kulingana na uamilifu wa kiusemi ambavyo ni: amri, taarifa, maswali na toleo vikiambatana na majibu yanayotarajiwa. Tuyafafanue hayo kwa jedwali lifuatalo.

**(1.2) Kielelzo cha Upokezano.**

| | Kuanzisha | Itikio | Pengine |
|---|---|---|---|
| Bidhaa/Huduma | kutoa | kupokea | Kukataa |
| | swali | jibu | nyamaza |
| | kudai | kuridhiwa | kukinai |

Katika kishazi kama upokezano, aina tofauti za sentensi zilitathminiwa kwa kutumia vigezo ambavyo tumeweka kwenye jedwali. Sentensi kama vile kanushi na za taarifa zilifafanuliwa. Tonisho ndiyo ilitumiwa kuziainisha kimaana. Hebu tufafanue mtazamo wa tatu wa kishazi ambao ni kishazi kama uwakilishi.

Uwakilishi wa kishazi unadhihirika kwa kubainisha ruwaza tofauti za tajriba. Kishazi ndicho kipashio ambacho kinatumika katika kuwakilisha mifanyiko au vitendo vinavyotekelezwa na akili zetu au vinavyofanyika katika ulimwengu tunamoishi. Sentensi sahili huwasilisha matendo, hisia, kuwapo kwa kitu au mtu. Haya yote yanaainishwa kwa mfumo wa kisarufi wa lugha na kuwakilishwa kupitia kishazi. Mifanyiko hii imedhihirishwa kwa kutambua mfanyiko wenyewe, wahusika na mazingira kwenye ule mfanyiko. Hebu tuyafafanue haya kwa jedwali lifuatalo.

**(1.3) Jedwali la Uwakilishi.**

| Kiwakilishi | Kijenzi |
|---|---|
| Mfanyiko | Kirai Tenzi |
| Mhusika | Kirai Nomino |
| Mazingira | Vielezi au Vihusishi |

Tuyafafanue maelezo haya katika kishazi kifuatacho huku tukionyesha vipengele husika na vitumizi vyake.

**(1.4) Mfano wa Kishazi cha Uwakilishi.**

| Kirai Nomino | Kirai Tenzi | Kirai Nomino | Kirai Elezi |
|---|---|---|---|
| *Mũnyambũ* 'Simba | *wasembethya* amekimbiza | *nau* baba | *mũno* sana' |
| Mhusika | Mfanyiko | Mhusika | Mazingira |

Kutokana na maelezo haya, kishazi kama uwakilishi kimebainishwa kama mhimili wa kutathmini mpangilio wa maneno katika sentensi za Kikamba na uamilifu wa kila neno katika kukamilisha usemi. Hata hivyo, hivi vishazi vitatu vina uwiano na amali lugha na tanzu za kisarufi.

Kishazi kama ujumbe kina uwiano na maana dhanishi na utanzu wa kisarufi wa semantiki. Amali lugha ya maana tagusani na utanzu wa pragmatiki nazo zinaoana na kishazi kama upokezano huku kishazi kama uwakilishi kikienda sambamba na maana matinishi na utanzu wa sintaksia. Uwiano wa mihimili mitatu ya kinadharia unaashiria ubora wa Sarufi Amilifu Mfumo, kwa minajili ya kuelekeza mbinu za utafiti.

### 1.9.0 Mbinu za Utafiti.

Mawanda mawili yaliyoshughulikiwa katika utafiti huu ni maktabani na nyanjani. Katika maktaba, mtafiti alisoma vitabu, majarida na tasnifu ili kupanua ujuzi wake kuhusu maana na matumizi ya tonisho. Zaidi ya hayo, utafiti maktabani ulikuwa muhimu kwa sababu ulimwezesha mtafiti kufahamu yaliyofanywa kuhusu mada hivyo basi kumwelekeza vizuri kwenye swala la utafiti na mada husika kwa jumla. Ujuzi huu ulichangia utaratibu wa utafiti nyanjani.

Utafiti nyanjani nao ulifanywa katika wilaya ya Machakos, tarafa ya kati. Machakos ndiyo makazi ya mtafiti na lugha ya Kikamba ndiyo inayotumika pale kwa wingi. Huko nyanjani hatua tatu zilifuatwa ili kufanikisha utafiti huu; kukusanya data, kuchanganua data na kuwasilisha uchanganuzi wa ile data kama matokeo ya utafiti. Data iliyokusanywa ni sentensi sahili na ilitambulika kwa kusikiliza na kuhusika kwenye mazungumzo.

### 1.9.1 Mbinu za Kukusanya Data.

Sentensi sahili zilizokusanywa kama data zilikuwa mwafaka katika uchanganuzi wa kisintaksia kwa sababu ziliweza kugawika kwa uwekevu hadi vipashio vidogo zaidi na kuonyesha uamilifu wa kila kipashio kwenye sentensi.

Aina tofauti za sentensi ambazo zilikusanywa katika utafiti huu ni za maswali, mshangao, taarifa, adabu, kukanusha, yakinishi na za amri. Ili kupata aina zote hizi za sentensi, tulitumia mbinu kama vile; mahojiano yasiyo rasmi, mtafiti kuhusika na kusikiliza huku akirekodi mazungumzo tofauti na pia kunakili hali tofauti za sentensi kama zinavyojitokeza (Kibrik 1977). Mahojiano yasiyo rasmi huwa bora (Mathooko 2004) kwa sababu wahojiwa huwa wametulia katika mazingira yao halisi na jambo hili huwafanya kuongea kikawaida tu.

Data ambayo ilikusanywa ilikuwa mazungumzo yaliyorekodiwa kuhusu mada tofauti na pia nakala ambazo zilinakiliwa na mtafiti. Kutokana na mazungumzo na mahojiano hayo, tuliweza kudondoa sentensi arobaini ambazo zilichanganuliwa. Kibrik (Ibid) anasema kuwa kongoo ya sentensi iliyo mwafaka kwa utafiti wa kisintaksia ni isiyozidi mia moja na isiyopungua sana. Hii ni kwa sababu sentensi nyingi zaidi huenda zikatatiza katika kuzichanganua.

Ukusanyaji wa data uliendelezwa kwa kutumia sampuli kimakusudi. Sampuli kimakusudi huteuliwa kwa kuchagua aina fulani ya watu ili kuwakilisha makundi



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

maalum katika jamii. Watafitiwa sita walichaguliwa; wanawake watatu, wanaume watatu. Hawa watafitiwa walikuwa baina ya umri wa miaka thelathini kufikia sitini. Umri huu ulitiliwa maanani kwa sababu inaaminika kwamba watu wa umri mkubwa huwa hawaathiriki sana na lugha zingine ilhali wale wachanga wanachanganya ndimi sana (Trudgill 1986). Nasi kwenye utafiti huu tulikusudia kulenga lugha moja ambayo ni Kikamba.

Kuna aina zingine za kusampuli lakini hazikutumiwa kwa utafiti huu kwa sababu sizingetoa sampuli wakilishi. Aina hizi za sampuli ni pamoja na sampuli makundi, sampuli kiwango na sampuli kimtandao (Orodho 2004). Sampuli makundi hutumiwa mahali ambapo watu ni wengi au wametapakaa eneo kubwa. Katika hali hii kundi lililoko karibu ndilo huteuliwa wala sio watu binafsi. Mfano mzuri ni wagonjwa wa ukimwi. Hawa wagonjwa ni wengi na ambapo sampuli inateuliwa mtafiti hachagui watu binafsi bali miji tofauti au hospitali tofauti katika nchi. Sampuli kiwango nayo inatumika katika kugawa watu katika viwango kwa misingi ya umri, vyeo au elimu. Sampuli kimtandao nayo hutumika ambapo kundi la kutafitiwa limesambaa na hakuna uwezekano wa kulileta pamoja. Mtafiti akitambua wachache wa hili kundi, anawatumia kuwapata wengine. Katika utafiti huu, aina hizi sizingetufaa kwa sababu tulikuwa tunatafiti katika uwanja wa sarufi na wala sio wa isimujamii.

### 1.9.2 Mbinu za Kuchanganua Data.

Data iliwakilishwa katika maandishi. Mazungumzo yalifasiriwa kwa lugha ya Kiswahili kwa manufaa ya msomaji. Kutokana na mazungumzo haya, aina tofauti za sentensi ziliteuliwa kwa mujibu wa uamilifu wake kisintaksia na kipragmatiki. Katika kigezo cha sintaksia, sentensi swalifu, arifu, kanushi, yakinishi na za amri ziliainishwa. Kwa upande wa pragmatiki, sentensi zenye dhamira tofauti ziliainishwa na kuelezwa. Sifa kama vile furaha, hasira, huzuni na uoga zilibainika kwa kusikiliza yale mazungumzo kwenye kinasasauti huku mtafiti akiyalinganisha na nakala alizokuwa ameziandika wakati wa kukusanya data.

Uchanganuzi mwingine uliangaza ruwaza za tonisho. Tonisho ndiyo iliyotuelekeza kujua sentensi ni za aina gani na zina uamilifu gani katika sarufi. Aina hizi tofauti za sentensi ziliambatanishwa na ruwaza tofauti za tonisho. Ilitambuliwa kuwa kila ruwaza ina dhima maalum kwa mujibu wa sentensi husika. Hivyo basi, aina tofauti za sentensi ziliambatanishwa na ruwaza tofauti za tonisho. Tonisho ilidhihirisha uamilifu wa kisintaksia na kipragmatiki.

### 1.9.3 Mbinu za Kuwasilisha Data.

Matokeo ya utafiti huu yaliwasilishwa kwa njia ya maelezo. Aina tofauti za sentensi zilipangwa kulingana na uamilifu wake na kwa mujibu wa matumizi ya ruwaza za tonisho. Haya yote yalidhihirishwa kupitia kwa mifano ya michoro iliyobainisha ruwaza tofauti za tonisho na aina tofauti za sentensi

zilizoambatanishwa nayo. Michoro ya matawi ilitumiwa kufafanua miundo ya sentensi tofauti na majedwali yalitumiwa kudhihirisha uamilifu wa ile miundo katika mawasiliano.

Taarifa muhimu iliyowasilishwa ni aina na dhima za maneno pamoja na virai vyake. Muundo na uamilifu wa sentensi katika Kikamba zilichanganuliwa kisha tonisho sintaksia na tonisho pragmatiki zikajadiliwa kwa kina katika sura ya tatu.

**Hitimisho**

Sura hii imefafanua usuli wa mada ya utafiti kisha ikaweka wazi suala la utafiti na malengo ya utafiti. Upeo na mipaka ya utafiti imewekwa na misingi ya kuchagua mada ikajadiliwa. Aidha, sura hii imehakiki maandishi kuhusu tonisho ya kijumla na ya Kibantu ambayo yameelekeza kulenga mada ya utafiti. Misingi ya kinadharia pia imemulikwa na kuwekwa wazi pamoja na mbinu za utafiti. Msingi huu umetuelekeza kuingia kwenye sura ya pili ambayo inaangaza muundo wa sentensi za Kikamba.

# SURA YA PILI

# MUUNDO WA SENTENSI ZA KIKAMBA

**Kitangulizi**

Katika utangulizi wa tasnifu hii (1.0) tulidokeza kwamba tungechunguza sarufi ya sentensi za Kikamba, kwa madhumuni ya kuchanganua na kufafanua uamilifu wa tonisho. Ni muhimu, kwa hivyo, kuchanganua pia muundo wa sentensi kimaumbo. Sentensi ni kipashio kikubwa kabisa cha kiimuundo ambacho hujumuisha vikundi vya maneno kama vile nomino, kiarifu na viambishi (Alex de Jola & Adrian Stenton 1980, Richards, Platt & Weber 1985, na Crystal 1987). Aidha vipashio vya kisarufi kama vile neno, kirai au kishazi hudhihirisha uamilifu wake kwenye kiwango cha sentensi. Hivyo basi, katika sura hii tutachunguza kategoria za maneno ya Kikamba.

## 2.1.0 Kategoria na Dhima za Maneno.

Ingawa Sarufi Amilifu Mfumo inatambua kuwemo kwa kategoria tofauti za maneno, nadharia hii haizingatii uainishaji wa haya maneno moja-kwa-moja. Nadharia iliyoshughulikia uainishaji wa maneno kwa utawalio ni ya Sarufi Zalishi (Radford 1997, 2004 na Tallerman 2005). Itakuwa bora basi kuainisha maneno ya Kikamba kwa kufuata mwongozo wa Sarufi Zalishi.

Katika mpangilio wa Sarufi Zalishi, maneno yaliwekwa kwenye kategoria nane. Kategoria husika zimetenganishwa makundi mawili: kundi la kileksia na kundi la kisarufi. Kuna kategoria tano ambazo ziliwakilishwa na Sarufi ya Mapokeo ambazo ndizo zimewekwa kwa kundi la kileksia.

(i) Nomino.

(ii) Vitenzi.

(iii) Vivumishi.

iv) Vielezi.

(v) Vihusishi.

Maneno ya kileksia yana sifa bayana za kisemantiki. Hivi ni kusema kwamba maneno haya huwakilisha maana msingi, tofauti na kategoria sarifu.

Kategoria sarifu ni mpangilio wa kategoria tatu za kimuundo (kisarufi) kulingana na marekebisho katika Sarufi Zalishi. Kategoria hizi ni;

(i) vibainishi.

(ii) shamirishi.

(iii) vipatanishi.

Kikundi cha maneno sarifu hakina maana msingi. Kinapata maana kupitia uamilifu kwenye sentensi (Radford 2004). Umuhimu wake mkubwa ni kuendeleza matumizi ya maneno mengine kwenye sentensi.

Kategoria zote nane zitajadiliwa kwenye kazi hii kwa sababu ndizo zitatumika kupambanua muundo wa sentensi. Kwanza tutajadili kategoria za kileksia kisha zile za kiuamilifu.

### 2.1.1. Nomino.

Nomino ni neno ambalo linatumika kutaja watu, vitu, mahali, hali au jambo lolote hata kama ni la kufikiriwa tu (Nkwera 1978). Nomino huweza kutambulishwa kwa vigezo vitatu ambavyo ni vya kisemantiki, vya kimofolojia na vya kisintaksia. Nomino zinapoainishwa kwa kigezo cha kisemantiki hupangwa kwa mujibu wa maana zinapoambatana na yale makundi yake.

**(2.1) Jedwali la Aina za Nomino Kisemantiki.**

| Nomino za | Kigezo | Jina | Maana |
|---|---|---|---|
| Dhahiri | Vitu vya kawaida: vinaweza kuwa na umoja na wingi. | *ĩvia – mavia*<br>*kĩvĩla - ivĩla* | 'jiwe' 'mawe'<br>'kiti' 'viti' |
| Dhahania | Vitu visivyoweza kuonekana au kushikika; vitu vya kufikirika au kudhaniwa. | *too*<br>*ũseo*<br>*ũuu* | 'Usingizi'<br>'uzuri'<br>'Upole' |
| Jumla | Vitu visivyoweza kuhesabika. | *Kĩw'ũ*<br>*Mũthanga*<br>*yĩia* | 'maji'<br>'mchanga'<br>'maziwa' |
| Jamii | Vitu ambavyo asili yake ni mkusanyiko au jamii ya vitu vyenye sifa moja. | *Muio wa ngu*<br>*Kikuthu kya nzwĩĩ* | 'tita la kuni'<br>'shungi la nywele' |
| Pekee | Majina ya watu au mahali maalum. | *Mũtũa,*<br>*Wanza*<br>*Kinya* | Mutua, Wanza<br>Kenya |

Utaratibu wa kimofolojia unazingatia viambishi vya umoja na wingi. Jedwali lifuatalo linaonyesha umoja na wingi wa nomino za Kikamba.

**(2.2) Jedwali la Nomino Kimofolojia.**

| Ngeli | Umoja | Maana |
|---|---|---|
| 1. | **mũ**ndũ | 'mtu' |
| 2. | **a**ndu | 'watu' |
| 3. | **mũ**tĩ | 'mti' |
| 4. | **mĩ**tĩ | 'miti' |
| 5. | **ĩ**tũ | 'jani' |
| 6. | **ma**tũ | 'majani' |
| 7. | **k**ĩveti | 'mwanamke' |
| 8. | **i**veti | 'wanawake' |
| 9. | **n**gũa | 'nguo' |
| 10. | **n**gũa | 'nguo' |
| 11. | **ka**mwana | 'mvulana' |
| 12. | **tu**mwana | 'wavulana' |
| 13. | **ũ**uu | 'upole' |
| 14. | **kũ**ĩa | 'kulia' |

Baadhi ya nomino hizi hubadilisha viambishi awali ambapo zinadhihirisha dhana ya wingi. Zingine zinabaki vilevile ziwe katika wingi au umoja. Umoja au wingi wa nomino hizo unadhihirika tu ambapo zinatumika kwenye sentensi. Hivyo basi, nomino hupangwa na kueleweka kwa misingi ya kisintaksia kama ifuatavyo.

**(2.3) Jedwali la Mpangilio wa Nomino Kisintaksia.**

| | Nomino | Mifano ya utapanisho | Visawe kwa Kiswahili |
|---|---|---|---|
| 1. | mũwau | ***Mũ*wau ũy*ũ* nĩ *waũ?*** | 'Mgonjwa huyu ni wa nani' |
| 2. | awau | *A*wau **a**ya *nĩ* ***ma**ũ?* | 'Wagonjwa hawa ni wa nani?' |
| 3. | mũvela | ***Mũ*vela nĩ **wa**temwa. | 'Mpera umekatwa.' |
| 4. | mĩvela | ***Mĩ*vela nĩ **ya**temwa. | 'Mipera imekatwa'. |
| 5. | ivuthĩ | **I**vuthĩ **y*ĩĩ*** **y*ĩ***vetwe. | 'Taka hii iondolewe'. |
| 6. | mavuthĩ | **Ma**vuthĩ **a**ya ***ma***vetwe | 'Taka hizi ziondolewe'. |
| 7. | kilalinda | **Kĩ**lalinda **kĩ**ngĩ nĩ ***ky*o**oka. | 'Kipofu mwingine amewasili'. |
| 8. | ilalinda | **I**lalinda **i**ngĩ nĩ ***sy*o**oka. | 'Vipofu wengine wamewasali' |
| 9. | nyũmba | **N**y*ũ*mba **ya**kana mwaki. | 'Nyumba imewaka moto' |
| 10. | nyũmba | **N**y*ũ*mba *sya*kana mwaki | 'Nyumba zimewaka moto' |
| 11. | kana | **Ka**na **ka**a nĩ ***ka***seo. | 'Mtoto huyu ni mzuri' |
| 12. | twana | **Tw**ana **tũ**ũ nĩ ***tũ***seo. | 'Watoto hawa ni wazuri' |
| 13. | uĩmi | **U**ĩmi **ũ**yũ ti ***mu***seo. | 'Ukulima huu si mzuri' |
| 14. | kũĩma | **Kũ**ĩma **kũ**ũ nĩ kwa kavinda. | 'Kulima huku ni kwa muda tu.' |

Kigezo cha kutambulisha nomino kisintaksia kinadhihirisha ni wapi katika sentensi nomino inapaswa kuwekwa na pia uamilifu wake kwenye ile sentensi. Kwa mfano, nomino inaweza kutumika kama kiima, jinsi inavyodhihirika katika kielelezo kifuatacho.



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

**(2.6) Nomino kama Chagizo**

Mwendwau aete *kĩw'ũ*. 'Shangazi ameleta maji'.

Nau aumaala *nza*. 'Baba ametoka nje'.

Kutokana na maelezo haya, tunaweza kuhitimisha kwa kusema kuwa, nomino ni kiungo muhimu katika sentensi. Nomino, hata hivyo, hazitumiki bila vitenzi.

## 2.1.2 Vitenzi.

Kitenzi ni neno ambalo hutokea kama sehemu ya kiarifu, na kawaida huambishwa mofu za njeo, hali, nafsi, idadi na dhamira (Richards, Platt & Weber 1985). Vitenzi huashiria vitendo au matukio kwenye sentensi. Katika hali isiyo ukomo, vitenzi vyote katika Kikamba huanzia kwa kiambishi *kũ* 'ku' ambapo maana inayojitokeza moja kwa moja ni kutenda jambo.

**(2.7) Vitenzi vya Kikamba.**

*kũya* – 'kula'

*kwina* – 'kuimba'

*kũsemba* – 'kukimbia'

*kũleela* – 'kuregea'

*kwona* – 'kuona'

*kũĩa* – 'kulia'

*kũĩma* – 'kukomaa'

*kũnoa* – 'kuchoka'

*kũvoya*- 'kuomba'

Vitenzi hivi vinapodondosha viambishi awali *kũ* 'ku' hutoa dhana ya kuamrisha. Aidha, umbo linalobaki huwa ndilo shina la kitenzi. Kitenzi kifuatacho kimetumia njeo, hali na nafsi tofauti.

**(2.8) Matumizi ya Nafsi, Hali na Njeo katika Vitenzi.**

*Nũkũya.* 'Anakula'

*Makaya.* 'Watakula'

*Nĩngũya*. 'Ninakula'

*Nĩtwaya.* 'Tumekula'

| Nafsi | Hali / Njeo | Shina |
|---|---|---|
| nũ – | - kũ - | - ya |
| ma – | - ka - | - ya |
| nĩ – | - ngũ - | - ya |
| nĩ – | - twa - | - ya |

*Kũ* 'na', *ka* 'ta', *ngũ* 'na' ni njeo ilhali *twa* 'me' ni hali timilifu.

Aidha, kuna mnyambuliko wa vitenzi (Munyao 2006). Vitenzi vinanyambuliwa kwa kuviongezea viambishi tamati ambavyo pia vinatoa maana tofauti ya kisarufi. Hivi ni vigezo vya kutambulisha vitenzi kimofolojia.

## (2.9) Mnyambuliko wa Vitenzi vya Kikamba.

| Kufanya | Kufanyia | Kufanyiana | Kufanyiza | Kufanyiwa |
|---|---|---|---|---|
| *Kũĩa*<br>'kulia' | *kũĩĩa*<br>'kulilia' | *kũĩanĩa*<br>'kuliliana' | *kũĩsya*<br>'kuliza' | *kũĩĩwa*<br>'kuliliwa' |
| *Kwina*<br>'kuimba' | *kwinĩa*<br>'kuimbia' | *kwinanĩa*<br>'kuimbiana' | *kwinĩthya*<br>'kuimbisha' | *kwinĩwa*<br>'kuimbiwa' |
| *Kũĩma*<br>'kulima' | *kũĩmĩa*<br>'kulimia | *kũĩmanĩa*<br>'kulimania' | *kũĩmĩthya*<br>'kulimiza' | *kũĩmĩwa*<br>'kulimiwa' |
| *Kũya*<br>'kuiba' | *kũyĩa*<br>'kuibia' | *kũyanĩa*<br>'kuibiana' | *kũyĩthya*<br>'kuibisha' | *Kũyĩwa*<br>'kuibiwa' |
| *Kũthooa*<br>'kununua' | *kũthooea*<br>'kununulia' | *kũthooania*<br>'kununuliana' | *kũthooesya*<br>'Kununulisha' | *kũthooewa*<br>'kununuliwa' |
| *Kũvanda*<br>'kupanda' | *kũvandĩa*<br>'kupandia' | *kũvandĩana*<br>'kupandiana' | *kũvandĩthya*<br>'kupandisha' | '*kũvandĩwa*'<br>'kupandiwa' |
| *Kũthamba*<br>'kuoga' | *kũthambĩa*<br>'kuogelea' | *kũthambĩana*<br>'kuogeleana' | *kũthambĩthya*<br>'kuogelesha' | *Kũthambĩwa*<br>'kuogelewa' |
| *Kũsemba*<br>'kukimbia' | kũsembea<br>'kukimbilia' | *kũsembania*<br>'kukimbizana' | *kũsembethya*<br>'kukimbiza' | *Kũsembewa*<br>'kukimbiwa' |

Katika Kikamba, vitenzi vinaambishwa mwanzoni na mwishoni mwa mzizi wa kitenzi ili kuunda sentensi. Kila mofu kwenye zile sentensi huwa na maana kisarufi. Chunguza mifano ya kauli hiyo.

## (2.10) Vitenzi Sentensi.


*Akamũũngamĩa.* 'Atamsimamia.'

*Nĩmanaendanisye.* 'Walienda pamoja.'

*Nĩwasembethwa.* 'Amekimbizwa.'

*Makaumaalany'a*. 'Watatoana nje.'

**(2.11) Kielelezo cha Kitenzi-Sentensi**




Mbali na vitenzi kutambulika kisemantiki na kimofolojia kuna kigezo cha tatu ambacho ni cha kisintaksia. Kisintaksia, vitenzi huwa na sifa ya kupangika mahali fulani kwenye sentensi. Kitenzi huwekwa baada ya nomino. Aidha, itategemea ni kitenzi cha aina gani ndivyo kikubalike kisintaksia kwenye ile sentensi.

Sehemu hii ya vitenzi imechambua uamilifu wa vitenzi katika sentensi za Kikamba. Sentensi bila kitenzi huwa haikamiliki wala haina maana. Kwa hivyo, kitenzi huwa kama nanga kwenye sentensi.

### 2.1.3 Vivumishi.

Vivumishi ni maneno yanayotoa taarifa zaidi kuhusu nomino (Richards, Platt & Weber 1985). Istilahi hii ya kivumishi inatokana na kitenzi kuvumisha ambacho kina maana ya kutoa habari zaidi. Katika Kikamba, tutachunguza vivumishi vya hali na sifa. Vivumishi hufuata nomino katika sentensi. Hata kama hazifuatani moja kwa moja, nomino wakati wote hutangulia kivumishi. Hiki ni kigezo cha kisintaksia cha kutambulisha vivumishi. Mifano ya vivumishi ni kama vile *mwanake*, 'mrembo', *nene*, 'kubwa', *mũasa*, 'mrefu' na *mũthwii,* 'tajiri.' Hebu tutungie sentensi vivumishi hivi.

**(2.12) Kielelezo cha Matumizi ya Vivumishi.**

Ula mwĩĩtu *mwanake* nũtwaiwe.

'Yule msichana mrembo ameolewa'.

Isũmba *ĩnene* ti *ĩseo*. 'Jumba kubwa sio nzuri.'

Mũtĩ *mũasa* nĩ watemwa. 'Mti mrefu umekatwa.'

Mũtumĩa ũla *mũthwii* anakwie ĩyoo. 'Mzee yule tajiri alikufa jana.'

Vivumishi vinaweza kuainishwa kwa mujibu wa uamilifu wake kama vile kitabia, umbo na hali. Tuchunguze jedwali la kufafanua haya.

**(2.13) Jedwali la Aina za Vivumishi.**

| Tabia | Umbo | Hali |
|---|---|---|
| *mũthũku* 'mbaya' | *mũnene* 'mkubwa' | *mũthwii* 'tajiri' |
| *mũseo* 'mzuri' | *mũmosu* 'mwembamba' | *ngya* 'maskini' |
| *mũkilu* 'mnyamavu' | *mũkuvĩ* 'mfupi' | *mũathime* 'mbarikiwa' |
| *mũtumanu* 'mjinga' | *mũasa* 'mrefu' | *mũtongoi* 'kiongozi' |
| *mũtulu* ' mvivu' | *mũnou* ' mnono' | *mũyo* 'tamu' |
| *mũĩ* 'mwerevu' | *mũtheu* 'safi' | *wũũ* 'chungu' |

Vivumishi vinaweza kufuatana viwili au vitatu kwenye sentensi moja (Radford 2004). Mifano ni kama ifuatayo kwenye sentensi.

**(2.14) Vivumishi Viwili au zaidi Kwenye Sentensi.**

Ula mwĩĩtu *mũasa mwanake* nĩwatwawa.

'Yule msichana mrefu mrembo ameolewa'.

Kĩla kĩvĩsĩ *kĩasa kĩnou kĩngũlũ* kĩĩva?

Yule mvulana mrefu mnono, mtukutu yu wapi?

Aidha, vivumishi vingine huchukua viambishi vya nomino husika. Huu ni mfano wa upatano wa kisarufi unaohusu pia matumizi ya maneno mengine yanayorejelea sifa fulani za kiima.

### 2.1.4 Vielezi.

Vielezi ni maneno ambayo hueleza zaidi kuhusu kitenzi, kivumishi au kielezi kingine. Kikamba aghalabu hutumia aina mbili za vielezi: vielezi vya kiasi na vielezi vya namna. Tuchunguze jedwali lifuatalo.

**(2.15) Jedwali la Aina za Vielezi.**

| Kiasi | Namna |
|---|---|
| *mũno* 'sana' | *mĩtũkĩ* 'haraka' |
| *nda* 'kabisa' | *kavola* 'polepole' |
| *vyũ* 'kabisa' | *mana* 'bure' |
| *vanini* 'kidogo' | *naĩ* 'vibaya' |
| *vaasa* 'mbali' | *nesa* 'vizuri' |

**(2.16) Vielelezo vya Vielezi katika Sentensi.**

Mwana ũyũ eanĩte *mĩtũkĩ.* 'Mtoto huyu amekua haraka.'

Mũndũ ũsũ nĩ mũasa *mũno* 'Mtu huyo ni mrefu sana.'

Atembeete kavola *vyũ.* 'Anatembea polepole kabisa.'

Yĩia yeanĩa *nda.* 'Maziwa yamejaa kabisa.'

Sũsũ aĩsaa *kavola.* 'Nyanya hula polepole.'

Vielezi katika Kikamba huwa havichukui viambishi vyovyote wala havigeuzi sentensi ziwe kwa wingi au kwa umoja. Kawaida, kisintaksia vielezi huwekwa mwishoni mwa sentensi. Kwa hivyo, vielezi vinaweza kutambulishwa kwa sentensi kulingana na mahali vilipowekwa. Hata hivyo, vielezi katika Kikamba ni vichache mno. Badala ya vielezi, vihusishi hutumiwa kwa wingi zaidi.

### 2.1.5 Vihusishi.

Vihusishi huonyesha uhusiano baina ya maneno mengine, kama vile nomino na kitenzi. Katika Kikamba, vihusishi huonyesha mahali jambo lilipofanyikia, na pia namna ambavyo limefanyika. Mifano ya vihusishi ni kama vile: *kwa* 'kwa', *wa* 'ya', *ya* 'cha', *ĩngĩ* 'tena', *nginya* 'mpaka', *vate* 'bila'. Tufafanue haya kwa sentensi zifuatazo.

**(2.17) Sentensi za Vihusishi vya Mahali.**

Kasũni ke ĩũlũ *wa* mũtĩ. 'Ndege yuko juu ya mti'

Mwaitu athi *kwa* mwĩĩtu wake. 'Mama ameenda kwa bintiye.'

Nau athi *nginya* ndũnyũ. 'Baba ameenda mpaka sokoni.'

Ivia yekw'a vakuvĩ *na* mwana. 'Jiwe limetupwa karibu na mtoto.'

Vihusishi vya kuonyesha jinsi jambo limefanyika hutumia kipashio '*na'*. Tuchunguze haya kwenye sentensi zifuatazo.

**(2.18) Vihusishi vya Namna.**

Aina *na* wasya mũnene. 'Ameimba kwa sauti kubwa'.

Mwendwau akw'a *na* thĩna mwingi. 'Ami amekufa kwa shida nyingi'.

Kwa wingi, vihusishi vinaeleza zaidi mahali kitendo kilipotendeka au jinsi kilivyotendeka. Haya yanatuelekeza kusema kuwa, vihusishi vina dhima ya kutoa ufafanuzi zaidi kwenye sentensi. Kisintaksia haya ni maneno ambayo yanawekwa baada ya vitenzi.

### 2.1.6 Vibainishi.

Vibainishi ni mojawapo ya maneno yenye uamilifu wa kisarufi. Katika sentensi, vibainishi ni maneno yanayotumiwa kurejelea nomino ili kuzitambulisha. Vibainishi vinaweza kuwekwa kabla ya nomino au baada ya nomino katika sentensi za Kikamba kutegemea ni vya aina gani. Vibainishi vinaweza kuwakilishwa na viwakilishi, vimilikishi, viashiria ama viulizi. Tuchunguze jedwali lifuatalo.

**(2.19) Jedwali la Vibainishi.**

| Viwakilishi | Vimilikishi | Viashiria | Viulizi |
|---|---|---|---|
| *ny'e* 'mimi' | *-akwa* '-angu' | *ũyũ* 'huyu' | *ata* 'nini' |
| *iIthyĩ* 'sisi' | *-itũ* '-etu' | *ũya* 'yule' | *nũũ* 'nani' |
| *we* 'wewe' | *-aku* '-ako' | *aya* 'hawa' | *va* 'wapi' |
| i*nywĩ* 'nyinyi' | *-enyu* '-enu' | *aaya* 'wale' | *ĩndĩĩ* ' lini' |
| *we* 'yeye' | *-ake* '-ake' | *asu* 'wao' | *kyaũ* 'nini' |
| *mo* 'wao' | *-oo* '-ao' | | |

**(2.20) Sentensi za Vibainishi.**

(i) *Ula* mwĩĩtu nĩ wathi mũsyĩ. 'Yule msichana ameenda nyumbani.'

(ii) *Kĩla* kĩvĩla kĩtũlĩku kĩĩva? 'Kile kiti kimevunjika kiko wapi?'

(iii) Mũndũ *ũsu* ti mũseo. 'Mtu huyo si mzuri.'

(iv) Maiũ *aya* nĩ meu mũno. 'Ndizi hizi ni mbivu mno.'

(v) Kũũ *kwake* ni kũtũlĩku. 'Mguu wake umevunjika'.

(vi) Wĩa *wake* nĩ mũseo. 'Kazi yake ni nzuri.'

(vii) *Nũũ* wooka kwitu? 'Nani amekuja kwetu?

(viii) Mwaitu easya *ata*? 'Mama anasema nini?

Sentensi za kwanza mbili (i & ii) zinaonyesha vibainishi vya kawaida. Hivi vibainishi huwekwa kabla ya nomino. Sentensi zinazofuata (iii & iv) zimetumia vibainishi viashiria ambavyo vinawekwa baada ya nomino. Sentensi za (v) na (vi) zimetumia vimilikishi ambavyo pia vinawekwa baada ya nomino. Sentensi (vii) na (viii) zimetumia viulizi. Viulizi vinaweza kuwekwa mwanzoni au mwishoni mwa sentensi kutegemea ni kiulizi cha aina gani.

Aidha, kimofolojia vibainishi huchukua mofu za nomino ambazo zimetumika isipokuwa baadhi ya vibainishi viulizi kama vile *ata* 'aje'. Maelezo haya yanaashiria kuwa, vibainishi katika Kikamba vina mahali pake kisintaksia kutegemea ni vya aina gani. Kwa hivyo, vibainishi vinarejelea nomino zinazotumiwa ili kuchukua maumbo yake. Vibainishi haviwezi kuelezeka kisemantiki lakini uamilifu wake unadhihirika kisarufi kwenye sentensi.

### 2.1.7 Shamirishi.

Shamirishi ni kategoria ya maneno ambayo hutumiwa kuanzisha vishazi tegemezi. Shamirishi huwa na uamilifu wa kutanguliza maneno mengine (Radford 2004). Aidha, shamirishi huwa na dhima ya kuonyesha kama kishazi inayotanguliza kina ukubalifu na vijenzi vyake kama vile kiima, idadi na nafsi. Hivyo basi shamirishi inaweza kutumiwa kubainisha kama kishazi ni swalifu au ni taarifa. Katika Kikamba, shamirishi ni maneno kama vile: *ethwa* 'ikiwa', *kwondũ* 'kama vile',

*ateo* 'ijapokuwa' miongoni mwa mengine. Hebu tuyachunguze kwenye sentensi zifuatazo.

**(2.21) Sentensi za Shamirisho.**

*Ethwa* nũkũka nĩngũmanya.

'Ikiwa atakuja nitajua.'

*Kwondũ wa* ũthũku wake, nĩwaũmanĩiwe.

'Kwa sababu ya ubaya wake, amelaaniwa.'

*Nĩkwĩthĩwa* nĩwooka, tũthi kwake.

'Kwa vile umekuja, twende kwake'.

Uamilifu wa shamirishi ni kuwekwa mwanzoni mwa vishazi. Shamirishi inapotumika hutambulisha kile kishazi kama tegemezi hivyo basi kualika kishazi kingine ili sentensi ikamilike kimaana na kisarufi pia.

### 2.1.8 Vipatanishi.

Vipatanishi ni maneno ambayo huwa na uamilifu wa kisemantiki wa kubainisha vijenzi vya kisarufi vinavyohusiana na vitenzi husika kama vile njeo, hali na azima (Radford, 2004). Vipatanishi hutofautiana na vitenzi leksia kwa sababu vinatumika kama visaidizi vyake kwenye sentensi. Katika Kikamba, maneno kama vile; *nĩenda* 'nataka', *nũtonya* 'unaweza', ni vipatanishi. Tunaweza kuwakilisha haya kwa sentensi kama ifuatavyo.



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

**(2.22) Kielelezo cha Sentensi za Vipatanishi.**

*Nĩenda* kũthi ndukanĩ. 'Nataka kwenda dukani'.

*Nũtonya* kũsemba vyũ. 'Unaweza kukimbia sana'.

Vipatanishi hutofautiana na vitenzi vya kawaida kwa vile vinakanushwa moja kwa moja kinyume na vitenzi vya kawaida. Hivyo basi, vipatanishi huchukua dhima ya ukanushaji kwenye sentensi.

Sehemu hii imechambua maneno leksia na maneno sarifu. Katika sentensi kunayo maneno ambayo huhusiana kwa karibu. Kwa mfano, nomino huhusiana na vivumishi, vitenzi huhusiana na vielezi navyo vibainishi na nomino. Maneno haya, katika kategoria mbalimbali huunganishwa ili kuunda kirai. Virai hivi hutegemea uhusiano huu wa maneno. Katika sehemu ifuatayo tutabainisha miundo virai kulingana na matawi katika sentensi. Miundo virai ndiyo huungana ili kuunda sentensi.

**2.2.0 Miundo Virai.**


Muundo wa sentensi unategemea uamilifu wa miundo virai. Virai ni vifungu vya maneno ambavyo huwakilisha vijenzi vya sentensi. Kwa mujibu wa Halliday (1985) na Radford (1997), kirai huundwa kwa njia sawa na sentensi sahili. Tutahakiki virai katika Kikamba kwa kurejelea nadharia ya Sintaksia Finyizi (Taz.

(Radford 2004). Sintaksia Finyizi, na Sarufi Zalishi kwa jumla huwakilisha muundo wa sentensi katika kielelezo matawi.

Miundo kirai katika Kikamba itadhihirishwa kulingana na majopo ya maneno manane ambayo tayari yamebainishwa. Ni kawaida ya miundo virai kuwakilishwa katika vifupisho kama: Kirai Nomino (KN), Kirai Tenzi (KT), Kirai Vumishi (KV), Kirai Elezi (KE), Kirai Husishi (KH), Kirai Bainishi (KB), Kirai Shamirishi (KSH) na Kirai Patanishi (KP). Sheria miundo virai huchanganua vipashio katika sentensi mpaka vile vidogo kabisa. Tufafanue kauli hii kwa tawi na upambanuzi ufuatao.

**(2.23) Kielelezo Matawi cha Muundo wa sentensi.**

*Andũ aingĩ mainaya lĩu.* 'Watu wengi hawakula chakula.'




$KP \rightarrow KN + P^1$

KN → N + B

$P^{1}$ → P + KT

KT →T + N

N → andũ

B → aingi

P → maina

T → ya

N → lĩu

Sheria za virai miundo pia huonyesha vipashio na uhusiano wake. Katika sentensi kunayo maneno ambayo huhusiana kwa karibu. Sheria hizi zitatolewa vielelezo vya matawi ili kufafanua ule uhusiano. Matawi haya huwa na sifa ya kugawika mara mbili (Adger 2003). Neno linalotangulia ndilo huwa neno kuu kwenye kile kirai.

Kwa kurejelea nadharia hii ya Sarufi Finyizi, tutahakiki miundo virai katika Kikamba kulingana na majopo ya maneno manane ambayo tumejadili. Tutachunguza kirai nomino, kirai tenzi, kirai vumishi, kirai elezi, kirai husishi, kirai bainishi, kirai shamirishi na kirai patanishi.

### 2.2.1 Kirai Nomino.

Kirai nomino ni kirai ambacho muundo wake umekitwa kwenye nomino au mahusiano ya nomino na neno au mafungu ya maneno. Kirai nomino kinaweza kuchukua sheria miundo zifuatazo:

KN → N

KN → N+V

KN → N+T

**(2.24) Vielelezo vya Kirai Nomino.**

*Sukulu* – 'shule'

KN

|

N

|

Sukulu

KN → N

N → sukulu

*Sukulu nzeo*. 'Shule nzuri'





KN → N+V

N → sukulu

V → nzeo

*Mwaitũ athi*. 'Mama aende'




KN → N+T

N → mwaitũ

T → athi

### 2.2.2 Kirai Tenzi.

Kirai tenzi ni kirai ambacho kimekitwa katika kitenzi au katika mahusiano ya kitenzi na neno au mafungu mengine ya maneno. Neno tawala katika aina hii ya kirai huwa ni kitenzi. Miundo ya virai tenzi inawakilishwa na sheria miundo virai zifuatazo.

KT → T

KT → T + E

KT → T + N

**(2.25) Vielelezo vya Kirai Tenzi.**


*Osa* . 'chukua'




KT → T

T → osa

*Semba mũno.* 'Kimbia sana'





KT → T+E

T → semba

E → mũno

*Una ngũ.* 'Okota kuni.'




KT → T+N

T → una

N → ngũ

### 2.2.3 Kirai Vumishi.

Kirai vumishi ni kirai ambacho muundo wake umekitwa katika kivumishi. Kwa kawaida, muundo huo huwa ni kivumishi na neno au fungu la maneno linaloandamana nacho. Virai vumishi vinachukua sheria miundo virai zifuatazo.


KV → V

KV → V + E

KV → V + E + E

**(2.26) Michoro ya Matawi ya Kirai Vumishi.**


*mwanake*. ‘mrembo’.




KV → V

V → mwanamke

*mwanake mũno*. ‘mrembo sana’.




KV → V+E

V → mwanamke

E → mũno

*mwanake mũno vyũ.* 'mrembo sana kabisa'.




KV → V+ $KV^1$

V → mwanake

$KV^1$ → V + E

V → mũno.

E → vyũ.

### 2.2.4 Kirai Elezi.

Kirai elezi ni kirai ambacho kinahusu maneno ambayo hufanya kazi kwa pamoja kama kielezi. Sheria za miundo virai zifuatazo zinatumika kwa virai vielezi.

KE → E

KE → E + E



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

**(2.27) Michoro ya Matawi ya Kirai Elezi.**


*mũno* – 'sana'




KE → E

E → mũno

*mũno vyũ.* 'sana kabisa.'




KE → E+E

E → mũno

E → vyũ

### 2.2.5 Kirai Husishi.

Kirai husishi ni kirai ambacho neno lake kuu ni Kihusishi. Katika Kikamba vihusishi huwa na muundo mmoja tu ambao ni kihusishi na kikundi nomino au kiwakilishi. Hebu tuchunguze vielelezo vifuatavyo.

**(2.28) Vielelezo vya Matawi ya Kirai Husishi.**


*vakuvĩ* – 'karibu'




KH → H

H → vakuvĩ

*vakuvĩ nake*. 'Karibu naye'




$KH \rightarrow H + KH^1$


H → vakuvĩ

KH$^{1}$ → H+B

H → na

B → ke

*ĩtina wa nyũmba.* ‘nyuma ya nyumba.’




KH → H+ KH$^{1}$

H → ĩtina

KH$^{1}$ → H+N

H → wa

N → nyumba

### 2.2.6 Kirai Bainishi.

Kibainishi kikitangulia katika sentensi huunda kirai bainishi. Tulisema kuwa vibainishi hujumuisha maneno kama vile viwakilishi, vimilikishi na viashiria. Sheria zifuatazo ndizo huwakilisha virai bainishi.

KB →B

KB →B+N

KB→B+B

**(2.29) Michoro ya Matawi ya Kirai Bainishi.**


*Ny'ie*. 'Mimi'




KB → B

B → ny'ie

*kĩla mũndũ*. 'kila mtu.'





KB → B+N

B → kĩla

N → mũndũ

*Ĩthyĩ ĩthyonthe*. 'Sisi sote'






KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

KB → B+B

B → Ĩthyĩ


B → ĩthyonthe

### 2.2.7. Kirai Shamirishi.

Maneno tawala kwenye virai hivi ni vishamirishi. Virai shamirishi huwa vikubwa kuliko virai vingine kwa sababu huundwa kwa kuunganisha shamirishi na kirai patanishi. Tuchunguze kirai kifuatacho.

**(2.30) Vielelezo vya Kirai Shamirishi.**

*kethwa nĩmeenda ũthi,* 'kama wanataka kwenda'.




KSH → SH+KP

SH → kethwa

KP → P+KT


KT → Ts+T

P → nĩme

Ts → enda

T → ũthi

*nĩkenda maende oyu.* 'ndiposa waende.'




KSH → SH+KP

SH → nĩkenda

KP → P+KT

P → ma

KT → T+E

T → ende

E → oyu

Shamirishi inapoanza sentensi hukusudia maelezo zaidi kwenye ile sentensi. Mifano ambayo tumetoa ingefafanuliwa zaidi kwa sababu neno shamirishi hualika


ufafanuzi kulingana na uamilifu wake kwenye sentensi. Tuhakiki virai patanishi navyo.

### 2.2.8 Kirai Patanishi.

Kirai patanishi ni kirai ambacho kipatanishi ndicho neno kuu. Tufafanue haya kwa mifano ifuatayo.

**(2.31) Vielelezo vya Kirai Patanishi.**

*Nĩenda ũthi ndũkanĩ.* 'Nataka kwenda dukani.'




KP → P+KT


P → nĩenda

KT → T+H

T → ũthi

H → ndũkani

*Nũtonya kwina nesa.* 'Anaweza kuimba vizuri.'




KP → P+KT

P → nũtonya

KT → T+E


T → kwina

E → nesa

Kirai patanishi huwa na dhima ya kujenga sentensi sahili kama inavyodhihirika kwenye vielelezo vifuatavyo.

**(2.32) Vielezo Ziada vya Virai Patanishi**

*(a)Nĩwathi mũũndanĩ.* 'Ameenda shambani.'




KP→ KN + $P^1$

KN → Ø

$P^1$→ P+KT


P → nĩwa

KT → T+H

T → thi

H → mũũndanĩ

(b) *Nĩwendete kũya.* 'Anapenda kula.'




KP→ KN+ $P^1$

KN → Ø

$P^1$→ P+KT

P → nĩwe

KT → T+T

T → ndete

T → kũya

Sehemu hii imedhihirisha virai vinane vya kileksia na kiamilifu mtawalia ambavyo ni: Kirai Nomino, Kirai Tenzi, Kirai Vumishi, Kirai Elezi, Kirai Husishi,

Kirai Bainishi, Kirai Shamirishi na Kirai Patanishi. Kwa upande wake, kirai patanishi ni sawa na kishazi au sentensi sahili katika misingi ya kisarufi. Kwenye sehemu ifuatayo, tutahakiki matumizi ya baadhi ya virai hivi tukizingatia uamilifu wake katika kishazi.

### 2.3.0 Uamilifu wa Vishazi.

Uamilifu katika sentensi sahili huelezwa kupitia istilahi kama vile kiima (K), kiarifu (Ki) na shamirisho (SH). Kiima ni sehemu ya sentensi inayotangulia kitenzi. Kiarifu nacho huja baada ya kiima na hutambulisha kinachotendwa na nomino. Shamirisho huwa ni sehemu ya mwisho kwenye sentensi inayoonyesha uhusiano wa moja kwa moja na kiarifu. Tunaweza kufafanua haya kwa kutumia sentensi sahili ya Kikamba.

**(2.34) Muundo wa Sentensi za Kikamba.**

Mwana nĩ wathi sukulu. 'Mtoto ameenda shule.'
(K) (Ki) (SH)


Kimsingi, sentensi yoyote ili iwe kamilifu kimaana sharti iwe na kiima ambacho huwakilishwa na nomino, na kiarifu ambacho ndicho hubeba ujumbe katika sentensi.

Maneno yanayowakilisha kiima na kiarifu katika kiwango kimoja yanaweza kuwa na uamilifu mwingine pia kwenye sentensi. Kwa mfano, nomino ambayo ina

uamilifu wa kiima inaweza kuwa na uamilifu pia wa mtendaji kwenye kishazi. Aidha, kitenzi ambacho kina uamilifu wa kiarifu kinapata uamilifu pia wa mfanyiko kwenye kile kishazi. Uamilifu huu unawakilishwa kwenye viwango tofauti. Tunaweza kudhihirisha haya kupitia sentensi na mchoro ufuatao.

**(2.35) Jedwali la Uamilifu wa Virai kwenye Kishazi.**

*Imwana syekya mavia.* 'Wavulana wametupa mawe.'




Nomino *imwana* 'wavulana' na *mavia* 'mawe' ziko katika kikundi kimoja lakini kila moja ina uamilifu tofauti katika sentensi kwa mujibu wa nafasi yake kisarufi. Haya yanatuwezesha kufafanua muundo wa kisarufi wa lugha yoyote.

Hata hivyo, katika sehemu hii, tutachunguza uamilifu wa sentensi za Kikamba kwa kurejelea amali lugha tatu ambazo tulizifafanua katika sura ya utangulizi wa kazi hii (Taz. 1.8.1). Amali husika zimechanganuliwa kuegemea mikabala mitatu, ambayo ni: kishazi kama ujumbe, kishazi kama upokezano na kishazi kama uwakilishi.

### 2.3.1 Kishazi kama Ujumbe.

Kimsingi, maudhui ndiyo sehemu tangulizi kwenye kishazi ikifuatiwa na kijalizo. Maudhui ni kile msemaji anachochagua kama mada ya usemi wake kwenye kile kishazi. Aidha, sio lazima maudhui yawe ni nomino au kirai nomino. Vijenzi kama vile kirai husishi au kirai bainishi vinaweza kuwa sehemu ya maudhui kwenye ujumbe. Kijalizo nacho ni sehemu inayokamilisha kishazi. Tuyachunguze haya kwa vielelezo vifuatavyo.

**(2.36) Vielelezo vya Sentensi za Maudhui katika Ujumbe.**

*Kĩvĩla kĩĩ nĩ kyatũlĩka.* 'Kiti hiki kimevunjika'

*Vakuvĩ nake vavaluka nzoka.* 'Karibu naye pameanguka nyoka.'

*We ndeũka ũmũnthĩ.* 'Yeye haji leo.'

**(2.37) Jedwali la Maudhui katika Ujumbe**

| Aina Kirai | Maudhui | Kijalizo |
|---|---|---|
| KN | *kĩvĩla kĩĩ* | *nĩ kyatũlĩka* |
| KH | *vakuvĩ nake* | *vavalũka nzoka* |
| KB | *We* | *ndeũka ũmũnthĩ.* |

Maudhui pia yanaweza kutambulika kwenye vishazi swalishi. Kimsingi, kishazi swalishi huuliza swali huku jibu likitarajiwa. Swali huulizwa ili jibu lipatikane. Hivyo basi, maudhui ya swali ni kile anayeuliza hutarajia kujibiwa. Kuna aina mbili za maswali; yanayotarajia majibu ya 'ndiyo/la' na yanayotarajia 'maelezo'. Kwenye maswali ya ndiyo/la ile sehemu ya kishazi inayoelekeza lile jibu ndiyo huwa ni maudhui. Tuyawakilishe haya kwa majedwali.

**(2.38) Maudhui katika Vishazi vya Maswali ya 'Ndiyo / La'.**

*Mwaitũ nĩwũkĩte?* 'Mama anakuja?'

*Mwana nũkũĩa?* 'Mtoto analia.'

| Maudhui | Kijalizo |
|---|---|
| *Mwaitũ*<br>*Mwana* | *Nĩwũkĩte?*<br>*nũkũĩa?* |

Katika maswali ya viswalishi, kipengele kinachobeba uamilifu wa maudhui ni kile kinachouliza lile swali. Sehemu swalishi ambayo inawakilishwa na maumbo kama: *nũũ* 'nani', *kyaũ* 'nini', *va* 'wapi', *meana* 'wangapi' na *ĩndĩĩ* 'lini' ndiyo huwa maudhui. Tufafanue hayo kwa jedwali lifuatalo.

**(2.39) Maudhui katika Maswali yenye Vibainishi.**

*Nũũ wũwaie kikombe?* 'Nani alivunja kikombe?'

*Nĩ kyaũ ũkwenda?* 'Ni nini unataka?'

| Maudhui | Kijalizo |
|---|---|
| *Nũũ*<br><br>*Nĩ kyaũ* | *wũwaie kĩkombe?*<br><br>*ũkwenda?* |

Katika kishazi amrifu, ujumbe wa kimsingi huwa, 'Nataka tufanye hivi' au 'Nataka ufanye hivi'. Kiini cha amri ni kutiiwa. Katika sentensi za Kikamba msisitizo katika amri huwa ni kile kitendo. Mtendaji hatajwi japo kipragmatiki, anafahamu ile amri ni yake. Hivyo basi, maudhui yake huwa tupu kulingana na vielelezo vifuatavyo.

**(2.40) Maudhui katika Vishazi Amrifu.**

*Umaala nza.* 'Tokeni nje'.

*Tuendei kyũmwa.* 'Twendeni kanisani.'

| Maudhui | Kijalizo |
|---|---|
| Ø<br><br>Ø | *umaala nza.*<br><br>*tuendei kyũmwa.* |

Hata hivyo, tumeweka msisitizo kwenye maudhui kwa sababu maudhui ndiyo hubeba ujumbe kwenye kishazi. Aidha, maudhui ndiyo hukipa kishazi mwelekeo wa umbo, kisarufi na kimuundo. Kishazi kama ujumbe kinahusiana na maana dhanishi pamoja na utanzu wa semantiki. Maana dhanishi kama amali lugha, ndiyo hubeba maudhui katika lugha. Utanzu wa semantiki nao ndio



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

unaoshughulikia kwa ujumla, mfumo wa maana katika lugha kama unavyoelezwa na sarufi na msamiati wake. Hivyo basi, vipengele hivi vitatu vinachangia kwenye ujumbe, na pia upokezano wa ujumbe.

### 2.3.2 Kishazi kama Upokezano.

Wakati ambapo kishazi kimepangwa kama ujumbe huwa wakati ule ule kimepangwa kimtagusano kati ya msemaji na msikilizaji. Katika kuongea msemaji anamhusisha msikilizaji ama kwa kutaka jibu kama ni swali au kwa kutarajia taarifa fulani (Halliday 1985). Hivyo basi, kishazi huwa na uamilifu wa kupokezana ambapo kinachukua miundo kama vile taarifa, maswali, au amri. Taarifa yoyote huhitaji kuitikiwa, maswali huhitaji majibu, na amri huhitaji kutiiwa. Kimsingi miundo yote hii ya mtagusano inahitaji itikio la kunena kando na kutenda linaloambatana na lile itikio. Tutatoa uamilifu wa kila kipashio kwenye sentensi. Istalahi kama kiima, kiarifu, shamirisho, chagizo, hali na salio zitatumiwa.

Istilahi za kwanza tatu zimeelezwa tayari (Taz.2.3). Chagizo huwa na uamilifu wa kuonyesha namna ambavyo shamirisho imeathirika. Hali nayo huonyesha sehemu ya sentensi ambayo inatambulisha kama sentensi ni aina ya taarifa, ni amri au ni swali. Salio nayo ni sehemu inayobaki baada ya kubainisha sehemu ya hali kwenye sentensi. Salio huwa aghalabu ni sehemu inayobeba shamirisho na

chagizo. Tutatumia majedwali kutolea mifano ya mtagusano kwenye miundo ambayo tumetoa ambayo ni taarifa, maswali na amri.

**(2.41) Kielelezo cha Upokezano katika Kishazi Arifu.**

*(a) Nau akũna mwana mũno.* 'Baba amempiga mtoto sana'.

*(b) Mwaitũ akooka ũnĩ.* 'Mama atakuja kesho'.

| Hali | | Salio | |
|---|---|---|---|
| Kiima | Kiarifu | Shamirisho | Chagizo |
| *Nau*<br>*Mwaitũ* | *akũna*<br>*akooka* | *mwana*<br>_ | *mũno.*<br>*ũnĩ.* |

Sehemu ya hali ndiyo ya maudhui kwenye vile vishazi na sehemu ya salio ndiyo shamirisho na chagizo, kama ipo. Kila kipashio kwenye vile vishazi kimepewa uamilifu wake. Kwa vile hivi ni vishazi vya taarifa, vinahitaji itikio kutoka kwa anayetolewa zile taarifa. Hatuwezi kuonyesha itikio lile kwenye majedwali kama vile tumeonyesha zile taarifa lakini ukweli ni kwamba kuna itikio kwenye kila kipokezano cha taarifa. Hebu tuchunguze upokezano kwenye kishazi amrifu.

Vishazi amrifu ni vishazi vinavyotoa amri. Amri hutolewa kwa mtu au watu walio karibu. Anayetoa hutarajia ile amri kutiiwa hivyo basi anapaswa kuwa katika nafasi ya mamlaka. Mwalimu anaweza kumtolea mwanafunzi amri au mwajiri mwajiriwa wake lakini sio kinyume cha haya. Mifano ya vishazi amrifu ni kama ifuatayo.

**(2.42) Vielelezo vya Vishazi Amrifu.**

*Kilya vyũ!* 'Nyamaza kabisa

*Ete lĩu mĩtũkĩ!* 'Leta chakula haraka!

*Sembai vyũ!* 'Kimbieni kabisa!'

Ili kuonyesha upokezano, vile vishazi vinaweza kuitikiwa kwa kusema *ĩĩ* 'ndiyo' au kwa kunyamaza tu na kutii kwa kufanya kile anayeelekezwa amri ameambiwa afanye. Tudhihirishe haya kwa majedwali yafuatayo.

**(2.43) Upokezano katika Kishazi Amrifu.**

*Kilya vyũ!* 'Nyamaza kabisa!'

*Ete lĩu mĩtukĩ!* 'Leta chakula haraka!'

*Inai nesa!* 'Imbeni vizuri.'

| Hali | Salio | |
|---|---|---|
| Kiarifu | Shamirisho | Chagizo |
| *Kilya* | _ | *vyũ* |
| *Ete* | *lĩu* | *mĩtukĩ* |
| *Inai* | _ | *nesa* |

Upokezano kwenye vishazi swalishi unaweza kudhihirishwa pia. Tutatoa mifano ya vishazi viswalishi aina zote mbili; vya kujibia 'ndiyo / la' na vinavyotumia vibainishi viulizi.

**(2.44) Upokezano katika Vishazi Swalishi**

(a) Vielelezo vya Vishazi vyenye Vibainishi.

*Nũũ waasya ngũa?* 'Nani amepoteza nguo?'

*Aĩva mwana?* 'Yuko wapi mtoto?'

(b) Vielelezo vya Vishazi vya Kujibu 'Ndiyo / La'.

*Nũũthi ndukanĩ?* 'Utaenda dukani?'

*Nũũka kwitũ?* 'Utakuja kwetu?'

Vishazi viswalishi huhitaji majibu yenye maelezo. *Nũũ* 'nani' ni kibainishi kinachohitaji jina la yule aliyetenda kile kitendo na pengine maelezo zaidi. *Aĩva* 'yuko wapi' vilevile ni kibainishi kinachohitaji ufafanuzi uliokurubiana na wa swali la kwanza. Kwenye vishazi vya 'Ndiyo / La', jibu linalohitajika tu ni 'ndiyo' au 'la.' Maelezo ni ya hiari na siyo muhimu. Hebu tuwakilishe haya kwa majedwali yafuatayo.

**(2.45) Upokezano kwenye Vishazi Swalishi.**

**(a)** *Nũũ waasya ngũa?* 'Nani amepoteza nguo?

*Aĩva nau?* 'Yuko wapi baba?'

| Hali | Salio | |
|---|---|---|
| Kiima | Kiarifu | Shamirisho |
| *Nũũ*<br>*Aĩva* | *Waasya*<br>_ | *ngũa?*<br>*nau?* |

**(b) Upokezano kwenye vishazi vya 'Ndiyo / La.'**

*Nũũthi ndukanĩ?* 'Utaenda dukani.'

*Nũkũka ũmũnthĩ?* 'Atakuja leo?'

| Hali | Salio |
|---|---|
| Kiarifu | Shamirisho |
| *Nũũthi*<br>*Nũkũka* | *ndukanĩ?*<br>*ũmũnthĩ?* |

Kwa kushadidia, kishazi kama upokezano kinaoana na utanzu wa kisarufi wa pragmatiki na amali lugha ya mtagusano. Vishazi ambavyo tumetoa kama mifano vimedhihirisha hali tofauti ambazo zimemulika muingiliano tofauti katika misingi ya sarufi kwa ujumla. Miingiliano hii itaendelea kujitokeza katika uchambuzi wa kishazi kama uwakilishi.

### 2.3.3. Kishazi kama Uwakilishi.

Kishazi kama uwakilishi kinahusu uamilifu wake katika maana matinishi inayooana na ruwaza za tajriba. Kimsingi lugha humwezesha binadamu kujenga taswira kwenye akili yake baina ya yale mambo yanayofanyika ulimwenguni na yale yanayoendelea akilini mwake (Halliday 2004). Katika hali hii, kishazi ndicho kipashio muhimu cha kuwakilisha taratibu husika.

Kuna taratibu tofauti katika lugha ambazo huwa na miundo tofauti ya kuwakilisha mifanyiko kwenye ile lugha. Njia ya kimsingi na ya kisintaksia ya kuwakilisha mifanyiko hujumuisha mfanyiko wenyewe, wahusika kwenye ule mfanyiko na mazingira ya ule mfanyiko. Mambo haya huweza kufasiri tajriba za kile kinachoendelea katika ulimwengu wa msemaji. Mfanyiko unawakilisha kile kinachoendelea, mhusika ni yule anayesababisha ule mfanyiko na mazingira ni mahali ule mfanyiko unapotekelezewa au jinsi unavyofanyika.

Dhana za mfanyiko, mhusika na mazingira ni kategoria za kisintaksia ambazo zinaeleza kwa jumla mambo kuhusu ulimwengu halisi kwa kuyawakilisha katika miundo ya kiisimu. Tutachunguza mifanyiko tofauti katika Kikamba iliyo na uamilifu maalum kwa mujibu wa aina zake. Kwanza tutatoa mfano wa hivi vipengele vitatu ambavyo vinahusiana kwa karibu na ile mifanyiko tutakayochunguza.

**(2.46) Vielelezo vya Uwakilishi wa Kishazi.**

(a) *Mwĩĩtu ainie mũno*. 'Msichana aliimba sana.'

*Mwana ooka oyũ.* ' Mtoto amekuja sasa.'

| Mhusika | Mfanyiko | Mazingira |
|---|---|---|
| Kirai nomino | Kirai Tenzi | Kirai elezi |
| *Mwĩĩtu* | *ainie* | *mũno* |
| *Mwana* | *ooka* | *oyũ* |

(b) *Mwĩĩtu auna ngũ kĩthekani.* 'Msichana ameokota kuni kichakani.'

*Ngĩtĩ yaũma kana mũno.* 'Mbwa amemwuma mtoto sana.'

| Mhusika | Mfanyiko | Mhusika | Mazingira |
|---|---|---|---|
| Kirai Nomino | Kirai Tenzi | Kirai Nomino | Kirai kihusishi |
| Mwĩĩtu<br><br>Ngĩtĩ | auna<br><br>yaũma | ngũ<br><br>kana | kĩthekani<br><br>mũno |

Tunasisitiza mifanyiko kwa sababu, kishazi kama uwakilishi kinawakilisha amali ya maana matinishi na utanzu wa sintaksia ambazo hujumuisha vitendo kwenye sentensi viwe halisi au vya kiakili. Kutokana na kategoria hizi za kisintaksia, tutachunguza mifanyiko yakinifu, mifanyiko ya kiakili na mifanyiko ya kiuhusiano.

Mifanyiko yakinifu ni mifanyiko ya kutenda. Mifanyiko hii inaeleza kwamba jambo fulani linafanyika kwa mtu/kitu fulani. Katika mifanyiko hii, yule anayefanya kile kitendo huitwa mtendaji na kama kuna mhusika mwingine kwenye ule mfanyiko, anaitwa mlengwa. Tutatoa mfano wa mfanyiko yakinifu wa mhusika mmoja na mfanyiko yakinifu wa wahusika wawili.

**(2.47) Kielelezo cha Mfanyiko Yakinifu**

(a) Mhusika mmoja.

*Nyamũ nĩyathaanyũka.* 'Mnyama ameruka.'

| Mtendaji | Mfanyiko yakinifu |
|---|---|
| *Nyamũ* | *nĩyathaanyũka* |

(b) Mfanyiko Yakinifu wa Wahusika Wawili.

*Nyamũ nĩyathaanyũkĩa kana.* 'Mnyama amemrukia mtoto'

| Mtendaji | Mfanyiko Yakinifu | Mlengwa |
|---|---|---|
| *Nyamũ* | *Nĩyathaanyũkĩa* | *kana* |

Katika kishazi cha kwanza kile kitendo kimekitwa tu kwa yule mnyama lakini katika kishazi cha pili, kitendo kimeelekezwa kwa mhusika mwingine ambaye ni mtoto. Ndiyo sababu maneno mlengwa au kilengwa yanatumiwa. Neno lingine linaloweza kutumiwa kwa uamilifu huu ni muathiriwa au kiathiriwa au kinachopitia ule mfanyiko (Tallerman 2005). Ubainifu wa dhima hizi unajijenga akilini.

Mifanyiko ya kiakili inahusu vitendo vinavyosababishwa na hisia. Vishazi vyenye vitendo hivi ni lazima viwe na mtendaji aliye na uwezo wa kutumia hisia kama vile kufikiri, kusisimka na pia kufahamu. Katika mifanyiko hii, tutatumia istilahi mhisaji na mhisiwa au kihisiwa kutegemea uamilifu wa yale maneno kwenye sentensi. Tuchunguze vielelezo vifuatavyo.

**(2.48) Vielelezo vya Mifanyiko ya Kiakili.**

(a) Mfanyiko kufuma Mhisaji na Kihisiwa.

*Ny'ĩe nĩĩwa naĩ.* 'Mimi najihisi mgonjwa!

| Mhisaji | Mfanyiko wa kiakili | Kihisiwa |
|---|---|---|
| *Ny'ĩe* | *nĩĩwa* | *naĩ* |

(b) Mfanyiko kufuma Mhisaji na Mhisiwa.

| Mhisaji | Mfanyiko wa kiakili | Mhisiwa |
|---|---|---|
| *Mwaitũ* | *nĩwendete* | *nau* |

Mifanyiko ya kiakili haiwezi kuwakilishwa kwa kutenda. Mifanyiko hii ni ya kiundani na ya kategoria tofauti na ile ya kiyakinifu. Aidha, mifanyiko ya kiakili sharti ionyeshe mhisaji na mhisiwa au kihisiwa ili ule mfanyiko ukamilike. Hebu tujadili aina ya tatu ya mifanyiko ambayo ni mifanyiko ya kiuhusiano.

Mifanyiko ya kiuhusiano inahusu umilisi wa hali au kitu fulani (Halliday 2004). Kila lugha huwa na taratibu zake za kueleza haya. Katika Kikamba, tunaweza kudhihirisha aina mbili za hii mifanyiko ya kiuhusiano: ya kuvumisha na kutambulisha.

**(2.49) Kielelezo cha Mfanyiko wa Kiuhusiano**

| Namna / Aina | Ya kuvumisha | Ya kutambulisha |
|---|---|---|
| 1. Kindani | *Umau nĩ mũĩĩ*<br>'Babu ni mwenye hekima.' | *Ũsũu nĩ mũtongoi*<br>'Nyanya ni kiongozi.' |
| 2. Mazingira | *Uthaithi nĩ Wakyumwa*<br>'Ibada itakuwa Juma pili.' | *Unĩ nĩ matukũ ĩkumi*<br>'Kesho ni tarehe kumi' |
| 3.Milikishi | *Mwĩĩtu ena ĩsoa*<br>'Msichana ana ushanga.' | *Isoa nĩ ya mwĩĩtu*<br>'Ushanga ni wa msichana.' |

Katika hali ya kuvumisha, ile sifa inahusishwa na mtu anayeimiliki. Aidha, inaweza kuwa sio mtu bali ni kitu. Hivyo basi tunatumia istilahi mbili ambazo ni mbebaji/kibebaji na kivumishi angama.

**(2.50) Kielelezo cha Mfanyiko wa Kuvumisha.**

| Sifa ya: | Mbebaji | Mfanyiko | Kivumishi - angama |
|---|---|---|---|
| Ubora wa ndani | *Mwaitũ* 'mama' | *nĩ* 'ni' | *mũseo.* 'mzuri'. |
| Mazingira | *Nau* 'Babu' | *e* 'yu' | *mũũndanĩ.* 'shambani'. |
| Umilikaji | *Mũũnda* 'Shamba' | *nĩ* 'ni' | *wa nau.* 'la babu'. |

Katika mifanyiko vumishi, mhusika huwa mmoja tu kwa sababu kivumishi kinachotumika pale sio mhusika. Kwenye mfanyiko vumishi unaoonyesha ubora wa ndani, mhusika anajumuishwa kuwa katika kundi fulani. Kwa mfano sentensi



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

*mwaitũ nĩ mũseo* 'mama ni mzuri' inadhihirisha kuwa mama yuko katika kikundi cha watu wazuri. Sehemu ya mazingira nayo inaonyesha uhusiano wa mhusika na kitu fulani au na mahali fulani. Umilikaji nao unadhihirisha hali ya kuwa na kitu fulani. Mifanyiko vumishi haiwezi kueleweka inapogeuzwa na kuandikwa kuanzia kwa kile kivumishi. Kwa mfano huwezi kusema *mũũndanĩ e nau* 'shambani yuko baba'. Jambo hili ni kinyume na mifanyiko tambulishi ambayo inaweza kueleweka na kutoa maana iliyokusudiwa hata kama itawakilishwa kwa kugeuza kwa kuanzia sentensi kwa neno la mwisho ambalo lina uamilifu wa kitambulisho.

**(2.51) Kielelezo cha Mfanyiko Tambulishi.**

| Utambuzi | Kitambulishwa | Mfanyiko | Kitambulisho |
|---|---|---|---|
| Kithamani | *Itheitũ* 'Babetu' | *nĩ* 'ni' | *mũtongoi* 'kiongozi' |
| Mazingira | *Unĩ* 'Kesho' | *nĩ* 'ni' | *Wathanthatũ.* 'Jumamosi.' |
| Umilikaji | *Mũũnda* 'shamba' | *nĩ* 'ni' | *wake* 'lake' |

Tunaweza kuwakilisha ile mifanyiko kutoka neno la mwisho kurudi la kwanza na itoe maana ili ile ambayo imo kwenye sentensi zilizomo kwa jedwali. Kwa mfano; tunaweza kusema;

*Mũtongoi nĩ ĩtheitũ.* 'Kiongozi ni babetu'

*Wathanthatũ nĩ ũnĩ.* 'Jumamosi ni kesho'

*Wake nĩ mũũnda.* 'Shamba ni lake'

Tofauti hii inatokana na kwamba, katika mifanyiko tambulishi, kitambulisho kinaweza kuwa na uamilifu wa kiima na kuanza ile sentensi. Mifanyiko vumishi haina sifa hii.

Kulingana na mjadala uliotangulia, kishazi kama uwakilishi kinatambulika kwa mifanyiko yakinifu, ya kiakili na ya kiuhusiano. Mifanyiko yote hiyo inawakilisha tajriba za binadamu za ulimwengu wake kama inavyodhihirika katika matumizi lugha. Lugha ndicho chombo kinachotumiwa kuwakilisha mifanyiko hii kupitia kwa kishazi.

**Hitimisho**

Sura hii imechanganua muundo na uamilifu wa sentensi za Kikamba. Muundo wa sentensi umebainishwa kupitia aina za maneno. Kategoria nane za maneno zimejadiliwa na kufafanuliwa kwa mujibu wa dhima zake katika Kikamba. Majopo mawili yameainishwa ambayo ni jopo leksia na jopo amilifu. Jopo leksia linajumuisha nomino, vitenzi, vivumishi, vielezi na vihusishi. Jopo amilifu nalo limesheheni vibainishi, shamirishi na vipatanishi. Majopo haya yalituelekeza kwenye muundo wa sentensi ambao ndio ulikuwa lengo kuu la sura hii.

Maneno nane yaliyojadiliwa ndiyo yalitumiwa kuunganishwa ili kuunda virai vya Kikamba. Tumebainisha virai vinane ambavyo ni kirai nomino, kirai tenzi, kirai vumishi, kirai elezi, kirai husishi, kirai bainishi, kirai shamirishi na kirai patanishi.

Michoro ya matawi ilitumiwa kwa kuwakilisha virai hivi. Michoro hii ilichangia kuonyesha uhusiano wa maneno kwenye vile virai. Miundo virai ilitumia mitazamo ya uzalishi kwa kuwa nadharia ya Sarufi Amilifu Mfumo huwa haizingatii miundo ya vishazi moja kwa moja.

Miundo virai ilituelekeza kwa uamilifu wa kishazi. Uamilifu wa kishazi ulidhihirishwa kupitia dhana za kiima, kiarifu, shamirisho, na chagizo. Dhana hizi zinaoana na umuundo ambapo kiima kinawakilishwa na kirai nomino, kiarifu kinawakilishwa na kirai tenzi, shamirisho nayo pia inawakilishwa na nomino ambayo inaathiriwa na kitenzi moja kwa moja, nayo dhana ya chagizo inawakilishwa na kirai kielezi. Uwiano huu ulitudokezea istilahi tatu za kishazi ambazo ni kishazi kama ujumbe, kishazi kama upokezano na kishazi kama uwakilishi.

Kishazi kama ujumbe kilifafanuliwa kwa misingi ya uamilifu wake wa kubeba maudhui. Uhusiano wa kishazi kama ujumbe na amali ya maana dhanishi na utanzu wa semantiki ulielezwa. Uamilifu wa kishazi kama upokezano ulidhihirishwa na uhusiano wake na amali ya maana tagusani na utanzu wa pragmatiki ukafafanuliwa. Kishazi kama uwakilishi ndio uamilifu wa mwisho uliofafanua mifanyiko tofauti. Uwiano kati ya kishazi kama uwakilishi na amali lugha ya maana matinishi pamoja na utanzu wa sintaksia zilijadiliwa katika sehemu hii.

Tunahitimisha kwa kusema kuwa, maneno leksia na meneno amilifu ni muhimu katika kuunda sentensi sarifu. Aidha, kila kirai huwa na muundo wake na ambavyo sheria ambatano katika Kikamba. Virai leksia ni vifupi kinyume na virai amilifu ni vikubwa kwa sababu ya uamilifu wake kwenye sentensi. Uamilifu wa virai katika Kikamba ni pamoja na kudhihirisha ujumbe na maana kamili, kuony esha uhusiano na pia kufafanua tajriba za watu kupitia mpangilio wa vile virai. Kikamba, kupitia virai, kinadhihirisha ukamilifu na uamilifu wa sarufi yake. Tuhakiki uamilifu wa tonisho katika sentensi za Kikamba katika sura ifuatayo.

# SURA YA TATU

# RUWAZA TONISHO KATIKA KIKAMBA

## Kitangulizi.

Katika sura ya kwanza, tulisema kuwa tunadhamiria kuchanganua uamilifu wa tonisho katika sentensi za Kikamba. Uchanganuzi huu unahitaji kudhihirishwa kupitia kwa ruwaza tonisho ambazo huwa na uamilifu maalum kwenye sentensi. Hivyo basi, sura hii itashughulikia ruwaza za tonisho sintaksia na tonisho pragmatiki.

## 3.1.0 Tonisho Sintaksia.

Sintaksia ni jinsi ambavyo miundo virai hupangwa ili kuwakilisha muundo na uamilifu wa sentensi (Tallerman 2005). Tonisho sintaksia inadhihirisha miundo tofauti ya sentensi kwa mujibu wa ushukaji au upandaji wa kidatu ambapo zile sentensi zinatamkwa. Muundo wa ruwaza za tonisho ambao tumetumia ni kutoka kwa waandishi kama vile Bolinger (1989) na Kimble – Fry (2001). Kwenye utafiti huu, tumeshughulikia aina tofauti za sentensi sahili ambazo miundo yake ni tofauti. Tumebainisha ruwaza za sentensi arifu, sentensi yakinishi, sentensi kanushi na sentensi ulizi

### .3.1.1 Tonisho katika Sentensi Arifu.

Sentensi zenye miundo ya kuarifu ni sentensi za taarifa. Sentensi za taarifa ni sentensi ambazo hudhihirisha kwa uwazi mpangilio wa kategoria za kiamilifu zinazohitajika katika sentensi (Aarts 1997). Kategoria hizi ni kama vile kiima, kiarifu na shamirisho. Katika sentensi hizi, kiima hutangulia kisha kiarifu na hatimaye shamirisho. Kwa kawaida, sentensi hizi hutumika kutoa taarifa. Katika Kikamba, sentensi za taarifa huwa zinadhihirishwa kwa tonisho ya kawaida. Ruwaza ya tonisho hii huanzia chini kisha inapanda katikati mwa sentensi. Kupanda na kushuka kwa ruwaza za tonisho hudhihirisha tonisho ya kawaida na hufafanua sentensi arifu. Kwa kawaida mtu anapozungumza hupandisha na kushukisha sauti. Sifa hii ya kushusha na kupandisha sauti huipa lugha zungumzwa utamu na dhima yake katika kufanikisha mawasiliano. Mchoro wa ruwaza hii ni kama ufuatao.

**(3.1) Kielezo cha Sentensi Arifu.**

*Nau nĩwooka mũsyi.* 'Baba amekuja nyumbani'.

**(3.2) Kielelezo cha Tonisho kwenye Sentensi Arifu.**



Tonisho inayodhihirika mwishoni mwa sentensi huwa chini zaidi ya mwanzoni. Jambo hili hutoa dhana ya kikomo cha ile taarifa. Aidha ule mpando huwa sio wa

juu sana na sauti huwa yenye uhakika. Mifano ya sentensi za taarifa katika Kikamba ni kama ifuatayo.

**(3.3) Mifano ya Sentensi za Arifa.**

*Mwanake nĩwathi mũũndanĩ.* 'Mvulana ameenda shambani'.

*Mwalimũ asomethya syana.* 'Mwalimu amefunza watoto.'

*Ngitĩ nĩyaũma ngũkũ.* 'Mbwa ameuma kuku'.

*Kana kaĩa mũno.* 'Mtoto amelia sana.'

Sentensi hizi zote zinachukua ruwaza ya tonisho ambayo imetolewa hapo juu kama kielelezo. Kama vile tumetangulia kusema, sentensi za taarifa aghalabu huwa na kategoria zote zinazounda sentensi za kawaida. Sifa hii ndiyo inazifanya ziitwe sentensi za taarifa kwa sababu zimewakilisha ujumbe kamili. Sentensi hizo nne tumetoa zimewakilisha kategoria ya kiima, kiarifu na shamirisho. Utamkaji wa sentensi hizi unachukua ruwaza ya tonisho ya chini, juu na chini zaidi. Hali hii ni tofauti katika sentensi ulizi.

### 3.1.2 Tonisho katika Sentensi Ulizi.

Sentensi za kuuliza kawaida huwa zinakusudia kupata taarifa fulani (Aarts Ibid). Kunazo taratibu mbili za maswali. Kuna utaratibu unaotegemea viswalishi na tonisho na utaratibu unaotegemea tonisho pekee. Taratibu zote hizi zipo katika Kikamba. Utaratibu unaotegemea viswalishi na tonisho unahitaji majibu ya

maelezo na tonisho inayoambatanishwa ni tofauti. Utaratibu wa maswali ya tonisho pekee ni maswali yanayotegemea majibu ya ‘ndiyo’ au ‘la’. Aidha, kwenye utaratibu huu kuna maswali yanayotarajia jibu moja baina ya mawili yaliyotolewa. Kwanza tutashughulikia maswali ya majibu ya ‘ndiyo’ au ‘la’.

Maswali yanayotegemea jibu la ‘ndiyo’ au ‘la’ huwa hayana viswalishi. Kueleweka kwake kama maswali kunategemea tonisho peke yake (Bokamba 1976). Katika Kikamba, tonisho ya maswali ya aina hii hupanda juu kabisa mwishoni mwa sentensi, na huwa na mpangilio wa maneno sawa na sentensi arifu lakini ruwaza ya tonisho inazitofautisha.

**(3.4) Kielelezo cha sentensi ya maswali ya ‘Ndiyo’/la’.**

*Nũũkua wĩ weka?* Utabeba peke yako?

**(3.5) Kielelezo cha Tonisho ya Maswali ya ‘Ndiyo’ /’La’.**



Tonisho hii huanza kawaida kisha inapanda juu zaidi kwenye neno la mwisho kwenye sentensi. Mifano zaidi ya sentensi za maswali ya aina hii ni kama ifuatayo.

**(3.6) Mifano ya Sentensi za Maswali ya ‘Ndiyo’/ ‘La’.**

*Ala angĩ nĩmokĩte?* ‘Wale wengine wanakuja?’

*Ũĩthyo wa ng'ombe nũyũ ?* 'Chakula cha ng'ombe ndicho hiki?'

*Nĩtĩũthi asala?* 'Tutapata hasara?'

*Sukuma nũũkaasyo?* 'Si sukuma utakuja nazo?'

Sentensi hizi hazihitaji majibu ya kuelezea. Mwenye kuulizwa lile swali anahitaji tu kusema 'ndiyo' au 'la'. Aidha, kwenye utaratibu huu kuna maswali yanayohitaji aulizwaye abainishe jibu kwa kuchagua majibu yaliyotolewa tayari. Aina hii ya maswali inaitwa maswali chaguzi

**(3.7) Maswali Chaguzi.**

*Wĩenda ngima kana nĩ ũsũũ?.* 'Unataka ugali ama uji?'

*Wĩthi unĩ kana nĩ aũke?* 'Utaenda kesho au kesho kutwa?'

*Ngũeno nĩ nzaũ kana nĩ ndune?* 'Nguo hii ni nyeupe au ni nyekundu?'

*Aĩsaa mĩtũkĩ kana nĩ kavola?* 'Yeye hula kwa haraka au pole pole?'

Majibu yanayotarajiwa kwa maswali haya yanategemea uchaguzi uliopewa ama jibu lingine linalokurubiana na yale lakini sio maelezo. Tonisho inayotumika ni ile ile ya maswali ya 'ndiyo'/'la' ambapo mwishoni mwa sentensi tonisho inapanda kabisa. Hivyo basi tunaweza kusema kuwa muundo wa sentensi za maswali unategemea majibu yanayotarajiwa. Hebu tuchunguze maswali yenye viswalishi.

Viswalishi ni maneno yanayotoa dhana ya kuuliza kama vile nani, wapi, lini, kwa nini, namna gani na mengine mengi. Kauli zenye viswalishi hutarajia maelezo anuwai kutegemea swali linahusu nini. Katika Kikamba, kauli zenye viswalishi hutumia maneno kama vile; *nũũ* 'nani', *va* 'wapi', *ĩndĩĩ* 'lini', *kyaũ* 'nini' *wakeana* 'lini', *nĩkĩ* 'kwa nini'. Sentensi hizi huchukua ruwaza ya tonisho iliyokaribiana na ya sentensi za maswali ya 'ndiyo'/'la' lakini inapanda kiasi mwishoni tofauti na ilivyo kwenye maswali ya 'ndiyo'/ 'la'. Aidha haianzii chini sana kama ilivyo kwenye sentensi arifu. Kielelezo cha ruwaza hiyo ni kama ilivyo hapa chini.

**(3.8.) Kielelezo cha sentensi za maswali yenye viswalishi.**

*Mwana akunwa nũũ?* 'Mtoto amepigwa na nani?'

**(3.9) Kielelezo cha Tonisho ya Maswali yenye Viswalishi.**



Ruwaza hii inaanzia juu kuliko ya maswali ya 'ndiyo'/ 'la', kisha inapanda ambapo kile kiswalishi kimewekwa. Maudhui ya lile swali huwa yamekitwa kwenye kile kiswalishi kwa hivyo tonisho inadhihirika zaidi mahali kipo na aghalabu huwekwa mwishoni mwa sentensi. Aidha, mkazo huwekwa kwenye kile kiswalishi.

**(3.10) Mifano ya Sentensi zenye Viswalishi.**

Syana syooka *ĩndĩĩ?* 'Watoto wamekuja lini?'

Nau aendete *va*? 'Baba anaenda wapi?'

*Nũũ* wavinga mũomo? 'Nani amefunga mlango?'

Mwana eĩa *nĩkĩ*? 'Mtoto analia kwa nini?'

Viswalishi vingine vinaweza kutangulia kwenye sentensi kutegemea ni vya aina gani. Kwa mfano, sentensi ya tatu imetanguliza kiswalishi. Hata hivyo inaweza kuandikwa kama ifuatavyo:

**(3.11) Kielelezo cha Sentensi Inayotumia Kiswalishi 'nani' Mwishoni.**

*Mũomo wavingwa nũũ?* 'Mlango umefungwa na nani?'

Ni wazi kuwa, kauli ya kitenzi imebadilika kutoka kauli ya kutenda na kuwa kauli ya kutendwa. Jambo hili halibadilishi ruwaza ya tonisho; inabaki vilevile. Kiswalishi kingine ambacho kinaweza kuwekwa mwanzoni mwa sentensi ni *nĩkĩ*' 'kwa nini'.

**(3.12) Sentensi zenye Viswalishi Mwanzoni.**

*Nĩkĩ* weeka ũu mwana? 'Kwa nini umefanya hivyo mtoto?'

*Nĩkĩ ũtekũya?* 'Kwa nini huli?'

Sentensi zingine zinawekwa viswalishi katikati na maana inabaki ile ile.

**(3.13) Sentensi zenye Viswalishi Katikati.**

Aendete *va* nau? 'Anaenda wapi baba?'



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

Nĩ *kyaũ* ũkwenda. 'Ni nini anataka?'

Nĩ *syakĩ* ngũa isu? 'Ni za nini nguo hizo?'

Viswalishi kama vile *wakeana* 'lini', *ĩndĩĩ* 'lini' *kĩ* 'kufanya nini' haviwezi kuwekwa mahali pengine kwa sentensi isipokuwa mwishoni tu. Ruwaza ya tonisho haibadiliki hata kiswalishi kikiwekwa wapi katika sentensi. Kile kinadhihirika ni mkazo unaowekwa kwa kile kiswalishi mahali kilipo tu. Tuchunguze sentensi yakinishi.

**3.1.3 Tonisho katika Sentensi Yakinishi.**

Sentensi yakinishi ni sentensi ambazo zinakubaliana na ukweli fulani. Kisintaksia, sentensi hizi huwa zinachukua muundo maalum katika Kikamba. Kwa madhumuni ya utafiti wetu, tumeshughulikia sentensi zenye kiima ili kuepuka sentensi za neno moja. Sentensi yakinishi hupandisha tonisho mwanzoni mwa mzizi wa kitenzi kinachobeba ile hali yakinishi.

**(3.14) Kielelezo cha Sentensi Yakinishi.**

*Mbũi nĩ kuya*. 'Mbuzi anakula.'

**(3.15) Ruwaza ya Tonisho ya Sentensi Yakinishi.**



Tuchunguze mifano ya sentensi yakinishi ili tuone miundo yake kisintaksia kutegemea njeo tofauti.

**(3.16) Mifano ya Sentensi Yakinishi katika Njeo ya Sasa:**

Mwana **nũkũĩa**. 'Mtoto analia'.

Ngitĩ **nĩkũ**kũma. 'Mbwa anabweka'.

Kaswii **nĩkaku**ĩtwe. 'Kifaranga anabebwa.'

**(3.17) Mifano ya Sentensi Yakinishi katika Njeo Ijayo:**

Mwĩĩtu ***aka***ina. 'Msichana ataimba'.

Kĩtanda ***kĩka***tũlĩka. 'Kitanda kitavunjika.'

Ngũa ***ĩka***vũwa. 'Nguo itaoshwa.'

**(3.18) Mifano ya Sentensi Yakinishi Njeo Iliyopita.**

Kĩmwana ***nĩkya***endie. 'Mvulana alienda.'

Mbũi ***nĩsya***sembie. 'Mbuzi walikimbia'.

Sukulu ***nĩya***vingiwe. 'Shule ilifungwa'.

Msisitizo kwenye sentensi yakinishi huwa katika sehemu ya kitenzi iliyobeba mzizi wake na ndipo tonisho hupanda ili kudhihirisha maudhui ya ile sentensi.

Njeo wala nafsi haziathiri ile ruwaza. Utaratibu huu unatofautishwa katika sentensi kanushi.

### 3.1.4 Tonisho katika Sentensi Kanushi.

Sentensi kanushi ni sentensi inayokana uyakinifu wa sentensi yakinishi. Kisintaksia sentensi kanushi huwa na muundo uliodhihirisha ukanushi wake. Sentensi za Kikamba hutumia vikanushi maumbo kulingana na njeo. Vikanushi maumbo hutegemea kiima kilichotumika au nafsi. Pia hutegemea sentensi ni ya umoja au ni ya wingi. Tonisho inayotumika kudhihirisha ukanushi inapanda kwenye kikanushi maumbo kisha inashuka.

**(3.19) Kielelezo cha Sentensi Kanushi.**

Nyie *ndĩ*ũthi. 'Mimi sitaenda.'

**(3.20) Kielelezo cha Tonisho ya Sentensi Kanushi.**



Sentensi kanushi na yakinishi zinatofautiana kwa ruwaza tonisho zinazotumika. Sentensi yakinishi hupandisha ruwaza kwenye mzizi wa kitenzi nayo kanushi hupandisha tonisho mahali kikanushi maumbo kinaanza na hii pia ni sehemu inayodhihirisha njeo na nafsi. Tutatoa mifano ya sentensi kanushi na maumbo tofauti ya ukanushi yanayodhihirika kupitia njeo na nafsi tofauti.

**(3.21) Sentensi Kanushi katika Njeo Iliyopo.**

| **Yakinishi** | **Kanushi** |
|---|---|
| Mwana *nũkũ*thi.<br><br>'Mtoto anatembea.' | Mwana *nde*ũthi.<br><br>'Mtoto hatembei.' |
| Kana *nĩkeũya*.<br><br>'Mtoto anakula' | Kana *kai*ũya.<br><br>'Mtoto hali.' |
| Ngũa *nĩkũ*vũwa.<br><br>'Nguo inaoshwa' | Ngũa *ndĩ*ũvũwa.<br><br>'Nguo haioshwi.' |

**(3.22) Sentensi Kanushi katika Njeo Iliyopita.**

| **Yakinishi** | **Kanushi** |
|---|---|
| Nau *nũna*nywie.<br><br>'Baba alikunywa.' | Nau *ndanee*nywa.<br><br>'Baba hakunywa'. |
| Kĩmwana *nĩkĩna*valũkile.<br><br>'Mvulana alianguka'. | Kĩmwana *kĩinee*valũka.<br><br>'Mvulana hakuanguka'. |
| Mũũnda *nũna*ĩmiwe.<br><br>'Shamba lilipaliliwa'. | Mũũnda *ndũnee*ĩmwa.<br><br>'Shamba halikupaliliwa'. |

Kikamba kinazo njeo bainifu za wakati uliopita nne na kila moja isipokuwa za kwanza mbili ina maumbo yake ya ukanushi yanayotegemea ile njeo. Tunaweza kuwakilisha njeo hizo kama ifuatavyo.

**(3.23) Vikanushi Kulingana na Wakati Uliopita.**

| | Wakati Uliopita | Yakinishi | Kanushi | Kikanushi |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Muda mfupi (saa) | Nau nĩwathi.<br>'Baba ameenda' | Nau ***ndana**athi.*<br>'Baba hajaenda.' | *ndana-* |
| 2. | Muda mrefu (kiasi cha siku moja). | Nau nũendie.<br>'Baba ameenda'. | Nau ***ndana**thi.*<br>'Baba hajaenda.' | *ndana-* |
| 3. | Muda mrefu (kuanzia jana). | Nau nũnaendie.<br>'Baba alienda'. | Nau ***ndanaa**thi.*<br>'Baba hakuenda.' | *ndanaa-* |
| 4. | Muda mrefu (kuanzia juzi kurudi nyuma). | Nau nĩwaendie.<br>'Baba alienda'. | Nau ***ndaa**thi.*<br>'Baba hakuenda'. | *ndaa-* |

Katika sentensi ya kwanza na ya pili, maumbo ya ukanushi ni sawa. Njeo hizo mbili zinakaribiana sana kiwakati kwa sababu kitenzi cha sentensi ya kwanza *nĩwathi* 'ameenda' kinaonyesha ameenda tu muda mfupi ambao umepita. Kitenzi cha sentensi ya pili, *nũendie* 'alienda' kinaonyesha kuwa alienda muda mrefu kiasi lakini siku hiyo hiyo. Vitenzi viwili hivi vinawakilisha matukio ya siku ile ile na ndiyo sababu vile vikanushi havijatofautiana. Miundo ya vikanushi na uyakinifu wa sentensi ni muhimu kwa sababu tonisho hupandishwa kwenye ile miundo ili kudhihirisha maana na umbo kisintaksia.

Sehemu hii ya tonisho sintaksia imechanganua sentensi arifu, sentensi swalifu, sentensi yakinishi na sentensi kanushi. Tumetambua kuwa muundo wa sentensi unazua ruwaza tofauti za tonisho ambazo zinawakilisha dhima tofauti katika sentensi. Miundo mingine ya sentensi inategemea tonisho peke yake ili kueleweka.

Hivyo basi, tonisho sintaksia ni dhima muhimu katika sarufi ya Kikamba. Tutaendelea kudhihirisha umuhimu wa tonisho kupitia dhima za kipragmatiki.

### 3.2.0 Tonisho Pragmatiki.

Pragmatiki ni matumizi na uchanganuzi wa lugha katika muktadha wa mawasiliano (Levinson 1993 na Yule 1996). Tonisho pragmatiki huwa na dhima ya kupasha ujumbe unaojitokeza kupitia ruwaza za kidatu katika sentensi na wala sio mpangilio wa yale maneno kwenye sentensi. Tonisho pragmatiki hutumika kufafanua dhamira tofauti za mawasiliano. Matumizi ya tonisho pragmatiki ndiyo yanayodhihirisha uamilifu wa sentensi katika mkutadha wa mawasiliano. Sentensi ambazo tutachanganua ni za dhamira amrifu, ya mshangao, ya huzuni, ya kusihi, ya kukejeli, ya kusisimua, ya hasira, ya uoga na ya ukakamavu.


### 3.2.1 Tonisho katika Sentensi zenye Dhamira Amrifu.

Sentensi amrifu ni sentensi ambazo hufasiriwa kuwa na dhamira ya kuamrisha (Aarts 2001). Tonisho ndiyo inayotumika kutoa zile hisia za amri. Mawasiliano katika hali hii yanaelekezwa kwa tonisho inayopandishwa na kushushwa huku msisitizo ukiwekwa kwenye kile kiwakilishi. Ruwaza ya tonisho hii huanza chini kisha inapanda na kushuka tena. Sentensi za ruwaza inayorejelea amri.

**(3.24) Sentensi Amrifu.**

*Ete ĩkanda we!* 'Leta kamba wewe!'

**(3.25) Ruwaza ya Tonisho katika Sentensi Amrifu.**



Ruwaza hii inaanza juu kiasi, kisha inashuka zaidi ya jinsi ilivyoanza. Amri inahusika sana na mtagusano kama tulivyotangulia kusema katika sura ya 'Muundo wa Sentensi', hivyo lugha ishara inatumika pamoja na tonisho hii ili kutiisha. Tonisho inapopanda na kushuka inaambatana na hizi ishara. Sentensi zaidi zenye dhamira hii ni kama zifuatazo.

**(3.26) Sentensi za Dhamira Amrifu.**

*Vaa vaikalike athoosya angĩ!* 'Hapa pasiingie wachuuzi wengine!'

*Nĩenda ũvoya we!* 'Nataka kuomba wewe!'

*Umaalai nza!* 'Tokeni nje!'

*Vindya ki!* 'Nyamaza kabisa!'

Sentensi ya kwanza ni ya muktadha wa kibiashara. Wale wachuuzi wanafukuzwa kwenye gari walimokuwa wakiuza bidhaa zao. Wanafukuzwa kwa kuwaghasi na kuwakinga abiria wanapoingia. Kauli yenyewe pia ina dhamira ya hasira kando na ile amri. Sentensi ya pili nayo inaelekezwa kwa mtu aliyekuwa akiongea anyamaze ili huyu msemaji (mhubiri wa mitaani) aombe aende zake. Amri hii ina kusudi la kumnyamazisha. Sentensi ya tatu nayo inakusudia kuondoa watoto wenye makelele nje. Sentensi ya nne ni ya kumnyamazisha mtu anayetoa ukelele

pengine wa usaidizi kwa sababu ya hatari ya kuvamiwa. Anayemwambia anyamaze ni jambazi na hivyo basi kauli yenyewe imejaa ukali na vitisho.

Sentensi zenye dhamira amrifu hazitolewi kwa kupaaza sauti tu bali ile tonisho hupanda na kushuka kwa ule mkazo mkuu. Anayeamrisha hukusudia kutiiwa kwa hivyo mkazo anaotumia unavuta nadhari ya anayeamrishwa kisha ile tonisho inamwelekeza msikilizaji kujua kuwa ile ni amri.

**3.2.2 Tonisho katika Sentensi zenye Dhamira ya Mshangao.**

Sentensi za mshangao huwa na muundo wa sentensi arifu isipokuwa pale ambapo kishangao kimetumiwa. Aidha, tonisho ya sentensi za mshangao hupanda juu mwishoni mwa sentensi kama ilivyo katika sentensi za maswali. Hata hivyo, kimuktadha wa mawasiliano, wanaohusika huelewana kuwa sio swali bali ni mshangao. Katika Kikamba maneno kama vile, *Iii* 'Akaa', *Asi* 'Ah', *Ata we* 'Aje', *Ivĩ* 'Ala' aghalabu hutumika pamoja na sentensi za mshangao. Hata yasipotumika, tonisho ya sentensi za mshangao hupanda mwishoni na dhamira yake inadhihirika tu. Hisia za mshangao zinajitokeza kwenye ile sauti na pia tonisho.

**(3.27) Sentensi yenye Mshangao.**

*Ula Nduku tyũũ!* 'Yule Nduku ni huyu!'

**(3.28) Ruwaza ya Tonisho katika Sentensi yenye Mshangao.**



Anayetamka sentensi hii haamini amemwona Nduku, rafiki yake. Inadhihirika umekuwa muda mrefu tangu waonane kwa hivyo ile kauli inakusudia kuwasilisha ujumbe huo. Hebu tuongezee sentensi zingine zenye dhamira ya mshangao.

**(3.29) Mifano ya Sentensi za Mshangao.**

*Asi, mwana akomie ĩmwe!* 'Ah, mtoto alilala fo!'

*Ivĩ, nowĩw'aa nthĩ!* 'Ala, kwani husikii!'

*Aĩ mwaitu nũendie kwoo!* 'Ati ma ma ameenda kwao!'

*Iii, etembea e mũthei! 'Akaa* anatembea uchi!'

Sentensi ya kwanza inatoa dhana ya kuwa mtoto alifariki. Hivyo basi sentensi hii ina dhamira ya mshangao na huzuni kwa sababu mtoto alilala na hakuamka tena (akafa). Sentensi ya pili nayo inadhamiria kukumbusha wazungumziwa jambo fulani. Msemaji alikuwa amewaambia wafanye jambo fulani na bado hawajafanya. Anashangaa ni kwa nini hawajafanya alilowaambia huku akiwakumbusha bado hawajalitimiza. Mfano mzuri ni watoto ambao wameambiwa watoke nje na bado wameketi mahali pale pale. Inabidi aliyewaambia atumie ile sentensi kwa dhamira ya kuwakumbusha na pia kushangaa ni kwa nini hawatii.

Sentensi ya nne nayo inadhamiria kutoa mshangao kwa ambapo msemaji amemwona mtu akitembea uchi. Sio kawaida kwa mtu mwenye akili timamu na mwenye heshima zake kutembea uchi. Kwa hivyo sentensi hii inadhamiria

kuonyesha jinsi msemaji haamini kuwa yule mtu anatembea uchi. Ni muhimu kusisitiza kwamba hata bila matumizi ya vihisishi ambavyo tumeweka mwanzoni mwa sentensi hizo, dhamira ya mshangao itajitokeza tu kupitia tonisho. Hivyo basi, sio lazima vile vihisishi kutumika.

### 3.2.3 Tonisho katika Sentensi zenye Dhamira ya Huzuni.

Huzuni husababishwa na matukio mabaya kama vile kifo, ugonjwa na mikasa mingine mingi. Mwenye kuhuzunika au kuathiriwa na huzuni atazitoa zile hisia kupitia kuzungumza kwake. Tonisho inayoambatana na huzuni ni ya chini hata kuliko inavyodhihirika katika kauli ya kiwango cha kawaida.

**(3.30) Sentensi yenye Huzuni.**

*Nĩtĩũkũvoyea mũno.* ‘Tutakuombea sana.’

**(3.31) Kielelezo cha Tonisho ya Huzuni.**



Sentensi zifuatazo ni mifano zaidi ya sentensi zenye dhamira ya kuwasilisha huzuni.

**(3.32) Mifano ya Sentensi za Huzuni.**

*Nũũvoa we.* ‘Utapona wewe!’

*Mũikamake.* ‘Msijali’

*Ithũmĩĩsye we.*'Jikaze tu!'

*Tũkoonana ĩngĩ.* 'Tutaonana tena!'

Sentensi zenye dhamira ya huzuni huwa na miundo mifupi mifupi na aghalabu huwa ni sentensi za neno moja ambalo ni kitenzi. Kwenye yale mawasiliano huwa kuna kuumia kwa moyo kwa hivyo mazungumzo huwa sio marefu. Kwa mfano, kwenye sentensi ya kwanza, anayeelekezwa ule usemi ni mgonjwa. Mzungumzaji anamtia moyo katika kule kuugua na ndiyo sababu anamwambia kuwa atapona tu. Kuna hisia za hofu kwa kuwa mara nyingi magonjwa huleta mauti! Katika sentensi ya pili kuna majonzi ya aina fulani. Wazungumziwa wanahimizwa na kufajiriwa pengine kwa sababu ya kufiwa au kwa sababu ya mkasa fulani.

Sentensi ya tatu iko na dhamira ile ile. *Ithũmĩĩsye* 'Jikaze' ni sentensi ya kutia mtu moyo kwa pigo fulani pengine la ugonjwa au kwa mkasa fulani. Sentensi ya mwisho nayo ina dhana ya kuachana kwa wanaopendana. Safari ya mbali inayofanya watu kutengana inahuzunisha maanake hawajui kama wataonana tena. Ukweli huu unawafanya kuhuzunika na kuagana kwa majonzi. Dhamira hiyo ndiyo inayojitokeza kwenye sentensi ya mwisho.

### 3.2.4. Tonisho katika Sentensi zenye Dhamira ya Kusihi.

Sentensi zenye dhamira ya kusihi huwasilisha dhana ya kushawishi au kubembeleza. Watu husihi wengine kwa dhamira tofauti. Kwa mfano, huenda

anayesihiwa anahitajika afanye hisani fulani ama asaidie kwa jambo fulani. Tonisho ya kusihi ni ya juu, chini na juu. Sauti yenyewe ni ya upole na yenye kuvutia. Katika Kikamba, maneno *mwa* 'tafadhali' na *naku* 'nawe' hutumika sana kwenye sentensi za kusihi. Lugha ishara pia hutumika sana kwenye sentensi za kusihi. Kusihi mtu sio jambo rahisi maanake huenda anayesihiwa asiwe na hisia au moyo wa kutenda anachoombwa atende. Watoto tu au watu wenye mioyo mikunjufu ndio huelewa na lugha ya kusihi. Tuchunguze ruwaza ya tonisho ya kusihi kwa kurejelea kauli ifuatayo.

**(3.33) Kielelezo cha Kauli yenye Kusihi.**

*Mwa naku ndũkathi.* 'Tafadhali nawe usiende.'

**(3.34) Kielelezo cha Tonisho ya Kusihi.**



Ruwaza ya tonisho ya kusihi hupanda ikishuka hata kama sentensi si sahili. Hebu tuchunguze sentensi zaidi zenye dhamira ya kusihi.

**(3.35) Mifano ya Sentensi za Kusihi.**

*Mwa mwana, ũka vaa.* 'Tafadhali, mtoto njoo hapa.'

*Vindya naku mwa.* 'Nyamaza nawe tafadhali'.

*Mwaitũ eteela o vanini.* 'Mama ngojea kidogo'.

*Ekai kũneenany'a nenyũ!* 'Wacheni kugombana nanyi'.

Katika sentensi ya kwanza, anayesihiwa ni mtoto. Anabembelezwa asongee karibu na mzungumzaji. Sentensi ya pili pia inaelekezwa mtoto au mtu anayelia. Anasihiwa akitarajiwa aache kulia. Nayo sentensi ya tatu inamsihi msikilizaji angoje kidogo tu. Pengine ni mteja anayehitaji kuhudumiwa naye mwuzaji anamshughulikia mwingine. Kule kumwita *mwaitũ* 'mama' ni kumheshimu na kumjali. Hiyo hali itamweka pale angojee kwa jinsi ambavyo ametambuliwa. Hii pia ni lugha adabu inayotambuliwa katika jamii ya Wakamba.

Sentensi ya nne nayo inawasihi watu wanaogombana waache. Mzungumzaji anatafuta amani baina yao kwa kuwaamua. Hivyo basi, sentensi zenye dhamira ya kusihi hulenga kugeuza nia za watu na kuwaelekeza kwingine. Mzungumzaji huenda akatiiwa kwa jinsi anavyotumia ile tonisho kufikia anaozungumza nao. Kauli hii ndiyo inatufanya tuseme tonisho hunena mengi kuliko yale maneno yaliyopangwa kwenye sentensi. Tuchanganue sentensi zenye dhamira ya kejeli.

### 3.2.5 Tonisho katika Sentensi za Kejeli.

Kukejeli ni tabia ya kuchezea mtu au kumtania. Dhamira hii ya kukejeli hujitokeza kibayana kwa sauti na kwa lugha ishara pia. Tabia ya utani hutumika hasa baina ya watu wanaohusiana kwa karibu au watu wa rika moja. Kwa mfano, tuchunguze usemezano baina ya msimamizi wa gari na mpakizi uwanjani wa magari.

**(3.36) Usemezano wenye Dhamira ya Kejeli.**

Msimamizi: *Kwata ĩkanda vau!*
'Shika kamba hapo!'

Mpakizi: *Nawaie mũongoĩ.*
'Nimeugua mgongo jameni'.

Msimamizi: *Wĩova wĩwĩte ũu!*
'Utafunga ukihisi hivyo.'

Mpakizi : *Nowĩ tei na ngya?*
'Huna huruma na maskini?'

Msimamizi: *Wĩa nĩ wĩa.*
'Kazi ni kazi.'

Mpakizi: *Nowĩwaa takwa.*
'Utaugua kama mimi.'

Msimamizi: *Nĩna mbesa ndina thĩna.*
'Nina pesa sina shida.'

Mpakizi: *Mbesa ti thayũ.*
'Pesa sio uhai.'

Kwenye usemezano huu, msimamizi ni mtu mwenye mamlaka pale na mpakizi anamtegemea kupata riziki yake. Aidha, wote ni watu wa rika moja. Yule mpakizi hana uwezo kiuchumi kwa hivyo atafanya ile kazi tu. Maneno ya msimamizi yamejaa kejeli. Ile tonisho ambayo imetumika pale ni ya juu mwishoni mwa sentensi. Tuchunguze kielelezo cha tonisho ya dhamira ya kejeli kama inavyorejelea kauli ifuatayo.

**(3.37) Sentensi yenye Dhamira ya Kejeli.**

*Kwata ĩkanda vau!* 'Shika kamba hapo'.

**(3.38) Kielelezo cha Tonisho ya Kejeli.**



Tonisho hii haianzii chini sana bali inaanza juu kiasi kisha inapanda zaidi. Imejaa kutothamini uwezowa mwingine.

### 3.2.6. Tonisho katika Sentensi zenye Hasira.

Hasira ni hali ya kughadhabika au kuwa na uchungu wa moyo kwa sababu ya kutoridhika na jambo fulani. Sentensi zenye dhamira ya hasira huanza kwa tonisho ya juu kisha hushuka mwishoni mwa sentensi na sauti huwa ya juu na msisitizo pia hutumika (Couper – Kullen 1986). Mzungumzaji mwenye hasira huzitoa kwa ukali hivyo basi ishara za mwili pia hutumika. Ile sauti huwa ya juu ili isikike na ujumbe upashwe. Kielelezo cha tonisho hii kinarejelea sentensi ifuatayo.

**(3.39) Sentensi yenye Hasira.**

*Ndũkaneeny'e ny'ie!* 'Usiongee na mimi!'

**(3.40) Kielelezo cha Tonisho yenye Hasira.**





KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

Tonisho hupanda na kushuka kisha kule kushuka kunachukuliwa na msisitizo. Kwa hivyo msisitizo huwa mwishoni mwa sentensi. Aidha mwendo wa sentensi za hasira huwa wa haraka haraka kwa sababu mzungumzaji anataka kumwaga yaliyomo moyoni mwake. Tutoe mifano zaidi ya sentensi za hasira.

**(3.41) Mifano ya Sentensi zenye Hasira.**

*Ndũkanosye we!* 'Usinichoshe wewe!'

*Mũikaaũke vaa kwakwa ĩngĩ!* 'Msije hapa kwangu tena!'

*Wĩenda kyaũ naku?* 'Unataka nini wewe?'

*Ndĩenda ngewa syaku!* 'Sitaki mambo yako!'

Sentensi yenye hasira huwa na uzito wa zile hisia za hamaki. Jambo hili linadhihirika kwa tonisho na lugha ishara. Sentensi ya kwanza inadhihirisha kuwa mzungumzaji amemkinai mwenzake na wala hataki uhusiano wake tena. Amemchosha tayari. Pengine kuna kitu anasisitiza kuitisha na jambo hilo limemsinya msemaji. Sentensi ya pili nayo inadhihirisha kuvunjika kwa uhusiano kabisa. Mzungumzaji anawafukuza na kuwapa onyo wasikilizaji kuwa wasirudi kwake tena. Sentensi ya tatu nayo inadhihirisha kuwa msemaji amemkinai mzungumziwa. Yule mzungumziwa lazima amemghasi msemaji mpaka hataki kumwona tena. Kule kurudi kwake pale ni kama kunamletea msemaji uchungu. Sentensi ya nne nayo inadhihirisha kuwa msemaji hata hataki kuongea na yule

mwenzake. Msemaji hataki kuhusika na kile msikilizaji anachohitaji au anachosema. Hebu tuchunguze tonisho katika sentensi zenye msisimko.

### 3.2.7. Tonisho katika Sentensi zenye Msisimko.

Msisimko katika muktadha huu tutaueleza kama hali ya kuleta hisia za furaha. Kusisimka husababishwa na habari njema au matukio mazuri ya kufaidi. Tonisho ya sentensi yenye msisimko huanzia juu kisha chini. Tonisho hii hupanda na kushuka kutegemea uzito wa msisimko wenyewe. Mwendo wake huwa wa kasi kwa sababu ya ule msisimko. Aidha, sauti yake huwa ya juu maanake huwa imeingia msisimko tayari. Kielelezo cha tonisho ya msisimko ni kama kinachodhihirika katika kauli ifuatayo.

**(3.42) Sentensi yenye Msisimko.**

*Nĩw'o nĩwooka nau!* 'Ni kweli amekuja baba!'

**(3.43) Kielelezo cha Tonisho ya Msisimko.**



Tonisho inaanza juu na kushuka kiasi tu kisha inapanda juu zaidi ya mwanzo. Hebu tuchunguze sentensi zaidi za msisimko.

**(3.44) Mifano ya Sentensi za Msisimko.**

*Ndyakwata wĩa!.* 'Nimepata kazi'.

*Nau akooka ũnĩ!* 'Baba atakuja kesho!'

*Mwaĩtu nĩwasyaa kamwana!* 'Mama amejifungua mvulana!'

*Mbaika nũvĩtie mtiani!* 'Mbaika amepita mtihani!'

Katika sentensi ya kwanza, msemaji anafurahia kupata kazi. Yaani haamini kuwa ameajiriwa kazi! Tonisho ya hiyo sentensi inaanza juu na kupanda juu zaidi kwa sababu sentensi hiyo ni ya maneno mawili tu. Sentensi ya pili nayo inapasha ujumbe wa mtu ambaye amekuwa hayuko na habari njema ni kuwa angewasili siku ifuatayo. Msisimko uliopo ni furaha ya huyo mgeni kuwa angekuja na pia kutoamini baada ya pengine, muda mrefu, angeweza kuja. Sentensi ya tatu nayo ina habari njema za mamake msemaji kupata mtoto wa kiume! Mtoto kuzaliwa kwenye jamii hii ni furaha na hasa mvulana. Sentensi ya nne inatoa habari njema za huyu msichana kupita mtihani. Tunakisia kuwa hakutarajiwa kupita lakini bahati imemwangukia. Hivyo basi, sentensi zenye dhamira ya msisimko hupasha ujumbe zaidi ya kile kimesemwa. Sentensi zenye uoga nazo zinatumia ruwaza tofauti.

### 3.2.8 Tonisho katika Sentensi zenye Uoga.

Kusababisha uoga ni hali ya kutia hofu. Tonisho ya sentensi zenye uoga hutegemea ujumbe unaopashwa na ile sentensi. Hata hivyo, nyingi ya sentensi hizi zinaanza kwa tonisho ya chini kiasi kisha inashuka zaidi. Mwendo wa kutamka

sentensi hizi pia ni wa kiasi tu wala sio wa kasi isipokuwa pale ule ujumbe unatisha. Mfano umo katika kauli hii.

**(3.45) Mfano wa Sentensi yenye Uoga.**

*Nzoka nĩsu kũũnĩ kwaku!* 'Nyoka huyo mguuni mwako!'

**(3.46) Kielelezo cha Tonisho katika Sentensi za Uoga.**



Sentensi kama hii inaogofya na kutisha pia. Kule kutishwa ndiko kunaingia kwenye nafsi ya msikilizaji kisha uoga nao unaingia. Iwapo kuna jambo la kuogofya, msemaji huwa makini kuupasha ule ujumbe kikamilifu kwa msikilizaji. Hivyo basi, hushukisha tonisho mwishoni mwa sentensi huku akiweka msisitizo. Tuchunguze mifano zaidi ya sentensi ya uoga.

**(3.47) Mifano ya Sentensi zenye Uoga.**

*Ve mũndũ wũkĩte!* 'Kuna mtu anakuja!'

*Nĩkũtukie na mwaitũ ndanoka!* 'Tayari ni jioni na mama hajafika!'

*Twĩĩsĩla va yu!* 'Tutapitia wapi sasa!'

*Umau ndanavoa.* 'Babu hajapona'.

Sentensi ya kwanza inatoa dhana ya kuwa wanaosemezana wako mahali pweke pasipo na usalama na wanaogopa huenda wakavamiwa na mtu asiye na kusudio nzuri. Msemaji kusema, *ve mũndũ wũkĩte* 'kuna mtu anakuja' ana lengo la kuwatahadharisha wenzake na pengine kuwafanya wanyamaze wasipatikane.

Sentensi ya pili nayo inatoa dokezo la kuwa kuna hatari. Huenda mama yuko hatarini kwa sababu usiku umefika na bado hajafika. Sentensi hii inatudokezea kuwa huyu mama hachelewi na hivyo basi lazima kuna jambo. Pengine kuna hatari imempata. Sentensi ya tatu nayo inaashiria hatari kwenye njia na hili linamfanya msemaji kuuliza wangepitia wapi. Pengine pale wanapopita kuna majambazi au mbwa wakali au chochote kile kinachohatarisha maisha yao. Sentensi ya nne ina ujumbe wa kuwa huenda babu akafa. Kule kutokupona kunaleta hofu kwa msemaji ya kuwa ule ugonjwa huenda ukasababisha kifo cha babuye. Hebu tuchunguze sentensi zenye dhamira ya ukakamavu.

### 3.2.9. Tonisho katika Sentensi zenye Ukakamavu.

Ukakamavu ni hali ya kutokubali kushindwa kwa urahisi. Hali hii inasababisha mhusika kuongea bila uoga na kueleza hoja zake kwa ujasiri na waziwazi. Msemaji huwa na uhakika wa jambo analolizungumzia na hajali nani anamsikiliza au kiwango cha mamlaka yake mradi hoja yake imemfikia. Tonisho ya sentensi zenye dhamira ya ukakamavu huwa ya juu na sauti pia huwa ya juu na dhabiti. Mwendo wake ni wa kasi lakini wenye umakini kwani huyu msemaji ni lazima aeleweke. Msemaji huwa na dhamira ya kutoa malalamishi au ujumbe fulani lakini anasikika ni kama anayeamrisha. Hebu tuwakilishe kielelezo cha tonisho yenye ukakamavu kwa kurejelea sentensi ifuatayo.

**(3.48) Sentensi ya Ukakamavu.**

*Ndienda wana wĩanĩ!* 'Sitaki utoto kazini!'

**(3.49) Kielelezo cha Tonisho ya Ukakamavu.**



Tonisho yenye ukakamavu huanza juu kisha inashuka chini kidogo na kupanda tena. Sentensi zingine zenye dhamira ya ukakamavu ni pamoja na:

**(3.50) Mifano ya Sentensi zenye Ukakamavu.**

*Twĩmũtavya uw'o wonthe!* 'Tutamwambia ukweli wote!'

*Nau ndetũthĩny'a.* 'Baba hatatusumbua.'

*Ndiũkĩa kĩndũ nyĩe!* 'Siogopi chochote mimi.'

*Twĩenda mũtalatalo ma maũndũ onthe.*

'Tunataka mpangilio wa mambo yote'.

Aghalabu, sentensi zenye ukakamavu huanza kwa kiarifu. Sentensi ya kwanza ina dhana ya kuwa kuna ukweli anayerejelewa hajajua na ndiposa msemaji anasema kuwa watamweleza yote. Ni wazi kuwa msemaji hajali matokeo baada ya ukweli ule kujulikana. Sentensi ya pili nayo inatuelekeza kuwa huyu baba ni msumbufu. Anasumbua watoto wake na mmoja wao ameamua kuwa atamkemea waziwazi. Kikomo cha ule usumbufu kimefika na ni wazi kuwa ataelezewa hayo! Sentensi ya tatu nayo ina maana ya kuwa, msemaji hajali wala haogopi. Lengo lake ni lazima

alitimize kulingana na mpango wake. Amekusudia na kuamua kuwa hakuna wa kumyumbisha au kumshawishi vingine. Sentensi ya nne inakusudia mambo yawekwe wazi. Msemaji anadokeza ya kuwa kuna mambo yaliyosetiriwa na hivyo basi mipango yote iwekwe wazi ili ikaguliwe. Pengine kuna ufisadi au uovu unaotendeka. Hayo yote yanategemea mkutadha wa zile sentensi na tonisho inayotumika.

Katika sehemu hii ya tonisho pragmatiki, tumeweza kuchanganua sentensi za Kikamba kwa kurejelea dhamira tofauti. Tulianzia na sentensi zenye dhamira amrifu, kisha zenye dhamira ya mshangao, dhamira ya huzuni, dhamira ya kusihi, dhamira ya kejeli, dhamira ya hasira, dhamira ya msisimko, dhamira ya uoga na mwishowe sentensi zenye dhamira ya ukakamavu. Tumechanganua maana iliyokusudiwa katika kila sentensi. Tumegundua kuwa, muktadha wa sentensi ni muhimu ili iweze kueleweka. Aidha, tonisho ni muhimu kwa kuweka wazi ile maana halisi ya sentensi. Muktadha wa ile sentensi unatambulisha maana kamili kwa mujibu wa mazingira ya matumizi yake.

Vilevile tumetambua kuwa kitenzi kimepata nafasi kubwa sana katika tonisho pragmatiki. Sentensi zenye dhamira ya ukakamavu, hasira, dharau, huzuni na amrifu zimeanza kwa kitenzi. Kitenzi hubeba nanga ya ujumbe wa sentensi na tonisho pragmatiki hujihusisha na ujumbe katika sentensi. Hivyo basi, kitenzi kimetumika ili kupasha ule ujumbe moja kwa moja.

**Hitimisho.**

Sura hii iliandikwa kwa madhumuni ya kubainisha dhima ya tonisho kwa misingi ya kisarufi. Kulingana na madhumuni haya, tumechanganua uamilifu wa tonisho sintaksia na tonisho pragmatiki. Uchanganuzi wa tonisho sintaksia umeshughulikia aina nne za sentensi ambazo ni; sentensi arifu, sentensi swalifu, sentensi yakinishi na sentensi kanushi. Tonisho imebainisha miundo ya sentensi hizi zote na kuzipa maana kisarufi. Uchanganuzi umedhihirisha kwamba kila matumizi yameandamana na ruwaza bayana.

Uchanganuzi wa tonisho pragmatiki umehakiki sentensi zenye dhamira tofauti. Umebainisha aina tisa za dhamira tofauti ambazo tumezitambulisha kwa ruwaza tofauti za tonisho. Zile sentensi zimetumika kuwasilisha ujumbe tofauti kulingana na mkutadha. Tumepitia sentensi zenye dhamira ya mshangao, dhamira ya huzuni, dhamira ya kusihi, dhamira ya kejeli, dhamira ya hasira, dhamira ya msisimko, dhamira ya uoga na dhamira ya ukakamavu. Tumetambua kuwa, tonisho pragmatiki inatuwezesha kufasiri semi za wasemaji pasipo wao kufafanua. Kwa mfano, sentensi zenye dhamira amrifu na mshangao zina tonisho inayokurubiana bali tofauti tunaitambua kwenye muktadha wa zile sentensi. Aidha, sentensi zenye dhamira amrifu, ya huzuni, ya hasira na ya ukakamavu zinakurubiana kisintaksia lakini ujumbe kipragmatiki kwenye kila aina ya sentensi ni tofauti.

Kwa mujibu wa matokeo hayo, tunaweza kuhitimisha kwa kusema kuwa, tonisho sintaksia na pragmatiki ni muhimu katika Kikamba. Aina hizi mbili za tonisho zinajenga mtagusano kupitia aina tofauti za sentensi za Kikamba. Mtagusano huleta mwingiliano baina ya msemaji na msikilizaji ambapo kuna maswali ya kujibiwa au amri za kutiiwa.

Aidha, tonisho pragmatiki imetubainishia umuhimu wa kutambua jinsi ambavyo usemi unatumiwa. Hivi ni kumaanisha kuwa kuna maana zaidi inayojitokeza kulingana na vile jambo linavyosemwa. Hivyo basi, mawasiliano hujumuisha kile ambacho kimesemwa na vile ambavyo kimesemwa. Vile kimesemwa hudhihirisha matumizi ya tonisho. Hivyo ni kumaanisha kuwa, tonisho ni kigezo muhimu katika sarufi ya Kikamba. Bila matumizi ya tonisho itakuwa ni vigumu kuelewana maanake ujumbe utakuwa haujakamilika.

Vilevile, imedhihirika kwamba kuna uwiano baina ya uamilifu wa tonisho na matumizi ya lugha ishara. Kule kuzungumza kwa sauti kali, nyororo, au shawishi, kunajumuika katika matumizi ya lugha ishara. Hivyo basi, matumizi ya tonisho hayawezi kutenganishwa na matumizi ya lugha ishara katika kukamilisha kuelewana kwenye mazungumzo.

# SURA YA NNE

# HITIMISHO

**Kitangulizi.**

Tulitalii usuli wa mada na suala la utafiti mwanzoni mwa kazi hii. Suala la utafiti lilifuatwa na malengo, maswali na tahadhania za utafiti. Sehemu hizi zilituelekeza kwenye upeo na mipaka ya utafiti iliyotuwekea wazi misingi ya kuchagua mada ya utafiti. Baadaye tulihakiki maandishi ya kijumla na ya Kibantu kuhusu tonisho. Tulijadili pia tafiti bayana za tonisho kabla ya kufafanua misingi ya kinadharia. Nadharia iliyotumika ni ya Sarufi Amilifu Mfumo kitengo cha mfumo maana. Baadaye tulihakiki mbinu za utafiti zilizojumuisha kukusanya, kuchanganua na kuwasilisha data.

Utafiti huu ulitekelezwa ili kuchunguza uamilifu wa tonisho katika sarufi ya Kikamba. Lengo la utafiti lilikuwa kubainisha ruwaza za tonisho katika sentensi za Kikamba pamoja na kufafanua uamilifu wake kwenye dhima za kisintaksia na kipragmatiki, tukikusudia kudhihirisha umuhimu wake katika sarufi ya Kikamba. Tulikusanya sentensi sahili arobaini kupitia mbinu ya kusikiliza na kushiriki mazungumzo anuwai kisha tukazichanganua kwa mujibu wa vigezo vya tonisho sintaksia na tonisho pragmatiki.

Mtazamo wa nadharia uliotumika wa Sarufi Amilifu Mfumo unazingatia lugha kama mfumo wa aina tatu za maana ambazo ni maana dhanishi, maana tagusani na maana matinishi, sawia na tanzu tatu za sarufi; semantiki, pragmatiki na sintaksia. Aina tatu za maana na za sarufi zinaoana na mitazamo mitatu ya kishazi ambayo ni kishazi kama ujumbe, kishazi kama upokezano na kishazi kama uwakilishi.

Ili kuhakiki aina nane za maneno yaliyotumika katika utafiti huu, tulitumia nadharia ya Sarufi Zalishi kwa mujibu wa Noam Chomsky. Katika kuchanganua misingi ya miundo virai kupitia vielelezo matawi, tulihusisha nadharia ya Sarufi Finyizi kulingana na mwandishi yuyo huyo. Ilitubidi tutumie nadharia hizi kwa sababu nadharia msingi ya utafiti huu, Sarufi Amilifu Mfumo, haishughulikii muundo wa sentensi licha ya kutambua dhana husika. Tusingeweza kuepuka kuchanganua aina za maneno na miundo virai kwa sababu hivi ni vijenzi vya kimsingi mno katika utafiti huu.

Mbinu za utafiti zilizotumiwa ni pamoja na kusoma maktabani na kukusanya data nyanjani. Kusoma maktabani kulimwezesha mtafiti kulenga suala la utafiti. Utafiti nyanjani ulichangia kupata sentensi sahili katika mandhari halisi ya wazungumzaji.Tulitumia sampuli kiwango kuteua data kisha tukaichanganua kupitia vigezo vya kisintaksia na kipragmatiki. Hatimaye tuliwasilisha data yetu kwa njia ya maelezo. Mbinu za uwasilishi zimebainisha matokeo ya aina mbalimbali kulingana na muhtasari ufuatao.



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

### 4.1.0 Matokeo ya Utafiti.

Kwenye sura ya pili, tulichanganua na kuwasilisha taarifa kuhusu aina na dhima za maneno. Majopo mawili ya aina za maneno ambayo ni jopo leksia na jopo sarifu yalibainishwa. Maneno katika jopo leksia ni: nomino, vitenzi, vivumishi, vielezi na vihusishi. Jopo sarifu nalo hujumuisha vibainishi, shamirishi na vipatanishi. Tulihakiki dhima ya kila aina ya maneno haya katika sarufi ya Kikamba.

Nomino huwa na dhima ya kiima, shamirisho na chagizo katika sentensi za Kikamba. Vitenzi navyo huwa na dhima ya kiarifu. Sentensi za kitenzi kimoja ni nyingi katika Kikamba na huwa zimekamilika kisarufi na kimawasiliano pia. Vivumishi navyo ni maneno yaliyo na dhima ya kuelezea zaidi kuhusu nomino huku vielezi vikifafanua zaidi kuhusu vitenzi, vivumishi na vielezi vingine. Dhima ya vihusishi vya Kikamba ni kuonyesha uhusiano baina ya maneno mengine katika sentensi. Vibainishi navyo hufafanua kinachohusiana na nomino kwa mujibu wa kinachoiwakilisha, inachomiliki, kiswalishi kinachoihusu, au kiashiria kinachoilenga. Shamirishi nayo ni maneno yanayoipa sentensi umbo kwa kurejelea mwanzo wake. Vipatanishi huwa na dhima ya kusaidia vitenzi vikuu katika kujenga sentensi sanifu.

Maneno haya yaliunganishwa kuunda virai katika Kikamba. Tulichanganua virai vinane vilivyojengwa kwa haya maneno manane. Tuliorodhesha na kuchanganua

kwa kutumia matawi virai vifuatavyo: kirai nomino, kirai tenzi, kirai vumishi, kirai elezi, kirai husishi, kirai bainishi, kirai shamirishi na kirai patanishi. Virai hivi vilitambulishwa kupitia kwa maneno tawala ambayo huitwa vichwa au maneno makuu. Ilidhihirika wazi kwamba, kirai nomino na kirai tenzi vina hadhi tukufu zaidi kuliko virai vingine. Kishazi chochote kile lazima kijumuishe virai hivi viwili ili kikamilishe ujumbe. Aidha, kirai patanishi kilibainika kuwa kijenzi sawa na sentensi sahili.

Muundo wa virai ulituelekeza kwa uamilifu wa vile virai. Katika sehemu hii tulitumia istilahi ya kishazi kwa sababu katika misingi ya kisarufi kirai kinaweza kuwa na maana ya kishazi. Aidha, nadharia msingi ya utafiti huu, Sarufi Amilifu Mfumo, inatumia istilahi hii kutambulisha uamilifu wa kishazi ambapo kishazi kimenasabishwa na uamilifu aina tatu. Uamilifu huu ni wa kishazi kama ujumbe, kishazi kama upokezano na kishazi kama uwakilishi. Tulifafanua uhusiano wa kishazi kama ujumbe na amali lugha ya maana dhanishi na utanzu wa kisarufi wa semantiki. Kisha tukahakiki kishazi kama upokezano na uhusiano wake na maana tagusani pamoja na utanzu wa pragmatiki. Kishazi kama uwakilishi kilioana na maana matinishi na utanzu wa sarufi wa sintaksia.

Kishazi kama ujumbe kilishughulikia vijenzi vya ujumbe ambavyo ni maudhui na kijalizo. Kishazi kama upokezano kilitambua mtagusano katika lugha unaowakilishwa na vishazi amrifu na swalifu. Kishazi kama uwakilishi huwa na

uamilifu wa kudhihirisha mifanyiko tofauti katika ulimwengu halisi wa binadamu. Tulihakiki mifanyiko mitatu ambayo ni mifanyiko yakinifu, mifanyiko ya kiakili na mifanyiko ya kiuhusiano. Uamilifu wa kishazi ulituelekeza kwa dhima ya tonisho katika sentensi za Kikamba, iliyochanganuliwa katika sura ya tatu.

Katika sura ya tatu tulihakiki uamilifu wa tonisho katika sentensi za Kikamba kwa kutumia vigezo vya tonisho sintaksia na tonisho pragmatiki. Kigezo cha tonisho sintaksia kilibainisha aina nne za sentensi tofauti. Tulihakiki sentensi arifu, sentensi ulizi, sentensi yakinishi na sentensi kanushi. Ruwaza tofauti za tonisho zilidhihirishwa kwenye kila aina ya sentensi hizi na kuambatanishwa na michoro yake. Sentensi arifu zilibainisha kuanza kwa tonisho ya chini kisha inapanda katikati ambapo kuna kitenzi halafu inashuka tena kwenye shamirisho. Sentensi ulizi nazo zina ruwaza ambayo hupanda mwishoni mwa sentensi. Ruwaza ya tonisho kwenye sentensi yakinishi imedhihirika kupanda mwanzoni mwa mzizi wa kitenzi kinyume na ruwaza ya sentensi kanushi ambayo hupandisha tonisho mwanzoni mwa vijenzi vya kile kitenzi ambapo kuna maumbo kanushi yaliyojumuisha njeo na nafsi kisha inaanza kushuka tena. Tonisho sintaksia inatumika sawia na tonisho pragmatiki.

Tonisho pragmatiki ilibainisha sentensi zenye dhamira tofauti. Sentensi zilizohakikiwa ni pamoja na sentensi zenye dhamira amrifu, ya mshangao ya huzuni, ya kusihi, ya kukejeli, ya hasira, ya msisimko, ya uoga na ya ukakamavu.

Ruwaza ya tonisho kwenye sentensi amrifu ilidhihirika kuanzia chini kisha inapanda na kushuka zaidi kuliko mwanzoni. Zile sentensi za mshangao nazo zilibainisha tonisho iliyopanda mwishoni mwa sentensi. Sentensi za huzuni zilibainika kwa tonisho iliyopanda na kushuka mwishoni mwa sentensi. Sentensi za kauli ya kusihi nazo zilidhihirisha ruwaza iliyopanda na kushuka na kupanda tena. Sentensi za kejeli zilibainisha ruwaza ya kupanda huku sentensi za hasira zikidhihirisha ruwaza ya kupanda na kushuka. Sentensi za msisimko nazo zilionyesha ruwaza iliyopanda, kushuka na kupanda zaidi kutegemea uzito wa ule msisimko. Ruwaza ya sentensi za uoga nayo ilichukua mkondo wa kupanda na kushuka kinyume na ya sentensi zenye ukakamavu ambayo ilidhihirika kupanda, kushuka na kupanda tena.

Huenda ruwaza zingine za tonisho katika sentensi hizi zilikurubiana lakini ni wazi kuwa, dhamira ya zile sentensi ilikuwa wazi kwa wasemaji na wasikilizaji. Kueleweka kwa zile ruwaza kulitegemea tu lugha zungumzwa. Aidha, tonisho pragmatiki ilibainisha waziwazi matumizi ya kitenzi kwenye sentensi zake. Aghalabu, tonisho ilipanda mahali pa kitenzi kwenye sentensi kudhihirisha umuhimu wa kitenzi. Kitenzi ndicho kinachoarifu kwenye sentensi na tonisho pragmatiki inashughulikia matumizi ya ujumbe ili kukamilisha mawasiliano. Hivyo basi, kitenzi kimetumiwa zaidi ili kusafirisha ule ujumbe moja kwa moja. Vile vile, pragmatiki hutumika kuwakilisha lugha katika muktadha wa mawasiliano. Kitenzi kimoja kinaweza kutumika kuwasilisha ujumbe kamili

kwenye yale mawasiliano. Mawasiliano haya hayakamiliki pasipo matumizi ya lugha ishara.

Aghalabu dhamira zote zilizochunguzwa zilijumuisha lugha ishara katika kuwasilisha ujumbe kamili. Dhamira ya kusihi ilidhihirika kwenda sambamba na matumizi ya mikono na kichwa. Dhamira ya mshangao nayo ilitumia ishara za uso na hasa kuinua nyuzi za macho na kukodoa macho. Uoga nao ulibainisha lugha ishara ya kujikunyata na hata kutetemeka kutegemea kinachoogopewa. Dhamira ya ukakamavu ilidhihirisha uso mkavu huku dhamira amrifu ikionyesha uso mkali. Hasira nayo ilionekana wazi kwa uso na kwa macho makavu huku huzuni ikidhihirika kwa macho yaliyolegea na matumizi ya mikono kushikilia kichwa kilichoonyesha uzito kwa sababu ya huzuni. Kutokana na maelezo hayo, tunaweza kubainisha mahitimisho ya utafiti huu.

**4.2.0 Mahitimisho ya Utafiti.**

Kutokana na muhtasari wa matokeo ya utafiti, tutahitimisha maelezo hayo kwa kusema kuwa, lugha zungumzwa ina mchango wake wa kisarufi ambao unajumuisha tonisho na sifa arudhi zingine. Asili ya lugha yoyote ile ni maneno. Katika kubainisha aina za maneno ambayo yanatumika katika kuunda sentensi za Kikamba, kitenzi kimedhihirika kuwa kijenzi muhimu sana kwenye zile sentensi. Hadhi hii inaafiki madai kwamba nanga ya ujumbe katika kishazi ni kitenzi.

Aidha, kishazi cha Kikamba kimedhihirisha uamilifu wa kupasha ujumbe, kupokezana na kuwakilisha tajriba za watu. Ukweli huu unatuelekeza kusema kuwa kishazi cha Kikamba kimekamilika kisarufi na kimawasiliano. Matokeo ya utafiti yamedhihirisha kwamba tonisho ni kipengele muhimu katika sarufi ya Kikamba na hakiwezi kupuuzwa. Kando na kipengele hiki kutia lugha hii nakshi pia kina umuhimu wa kutoa maana zaidi ya yale yamesemwa.

Imebainika pia kuwa, tonisho kama kipengele cha sarufi hakifunzwi kwa mwenyeji wa lugha hii bali anakipokea tu kama vipengele vile vingine vya sarufi. Mwenyeji wa Kikamba hafikirii aweke tonisho ipi wapi ndiyo ibainishe ujumbe fulani bali anaitumia tu kikawaida. Hivyo basi, matumizi ya tonisho ni mojawapo ya vipengele vya ujuzi wa kisarufi. Ujuzi kama huo umejisawiri katika ubongo wa msemaji, na kushirikiwa na wenyeji wote wa lugha.

Vilevile, tumetambua kuwa tonisho pragmatiki ni pana sana. Tumewakilisha sentensi zenye dhamira tofauti chache tu lakini kile kigezo ni kipana mno. Kikamba kinaweza kuzua dhamira zaidi kwa mujibu wa lugha zungumzwa. Aidha, tonisho sintaksia na tonisho pragmatiki huenda sawia. Hatuwezi kuzitenganisha kikawaida tunapozungumza. Imetubidi tuzitenganishe kwa madhumuni ya mpangilio wa kazi yetu. Labda uhusiano dhabiti utahitaji utafiti zaidi.

### 4.3.0 Mapendekezo ya Utafiti Zaidi.

Utafiti zaidi unaweza kufanywa ili kutambua kama kuna ruwaza za tonisho zinazokurubiana na sababu za ule ukuruba. Utafiti wa aina hii pia huenda ukabainisha kwa uwazi kinacholeta tofauti ya zile ruwaza na hasa wazungumzaji wanapoongea. Jambo hili linatuelekeza kwa utafiti zaidi kuhusu uhusiano wa tonisho na lugha ishara katika Kikamba.

Tulitambua mwingiliano mkubwa wa lugha ishara ambapo tonisho ilitumika kutoa ujumbe fulani. Huenda utafiti kama huu ukatambua aina fulani za lugha ishara ambazo zinaambatana na ruwaza maalum za tonisho. Aidha, utafiti zaidi unaweza kufanywa kuhusu mkazo na jinsi unavyohusiana na tonisho katika Kikamba. Kuna ukuruba mkubwa baina ya sifa arudhi mbalimbali katika matumizi ya lugha zungumzwa. Utafiti juu ya mkazo na tonisho unaweza kubainisha wazi zaidi uamilifu wa kila moja kwenye sentensi.

Utafiti huu una nafasi ya kuchangia katika sarufi ya Kikamba kwa kuchanganua ruwaza za tonisho katika sentensi. Mchango huu umejikita katika uwanja wa sintaksia na hasa katika misingi ya nadharia ya kisasa ya Sarufi Amilifu Mfumo. Matokeo ya utafiti huu yanaweza kutumika katika ufundishaji wa Kikamba kama lugha ya Kiafrika. Vile vile, utafiti huu utachangia katika kudhihirisha uwezekano wa tafiti katika mapendekezo yaliyotolewa kwa hivyo zina nafasi ya kukuza nadharia ya isimu jumulifu pamoja na isimu tumikizi.

## MAREJELEO


Aarts, B. 2001. *English Syntax and Argumentation*: 2nd Ed. New York: Palgrave Publishers Ltd.

Adger, D. 2003. *Core Syntax. A Minimalist Approach*. New York: Oxford Unversity Press.

Alex de Jola & Adrian Stenton 1980. *Terms in Systemic Linguistics – A Guide to Halliday*. Batsford: Academic & Educational Ltd.

Armstrong, E. L. 1967. *The Phonetics & Tonal Structure of Kikuyu Grammar*. London: International Africa Institute by Dawsons of Pall Mall.

Ashton, E.O. 1944. *Swahili Grammar: Including Intonation*. London: Longman Ltd.

Bokamba, E.G 1976. Question Formation in some Bantu Languages. Ph.D Thesis. Indiana University.

Bolinger, D. 1968. *Aspects of Language*. New York: Harcourt, Brace & World Inc.

Bolinger, D. (ed.) 1972. *Intonation*. England: Penguin Books Ltd.

Bolinger, D. 1989. *Intonation & Its Uses: Melody in Grammar & Discourse.* London: Edward Arnold Publishers Ltd.

Brazil, D. 1980. *Discourse Intonation & Language Teaching.* London: Longman Group Ltd.

Crystal, D. 1985. *Dictionary of Linguistics & Phonetics*: 2nd Ed. Cambridge: Basil Blackwell Ltd.

Crystal, D. 1987. *The Cambridge Encyclopedia of Language.* Cambridge. Cambridge University Press.

Couper-Kuhlen, E. 1986. *An Introduction to English Prosody.* London: Edward Arnold Publishers Ltd.

Cruttenden, A. 1986. *Intonation*: 2nd Ed. England. Penguin Books Ltd.

Guthrie, M. 1948. *Collected Papers on Linguistics.* London: Oxford University Press.

Guthrie, M. 1967. *Classification of Bantu Languages.* London: Dawisons of Pallmall.

Finch, G. 2000. *Linguistic Terms & Concepts.* Bristol: Palgrave Macmillan.

Ford, K.C. 1974. Tone & Intonation in Kikuyu. A Research Paper. University of Nairobi.

Ford, K.C. 1975. Tone & Intonation in Kikamba. A Research Paper. University of Nairobi.

Habwe, J. & P. Karanja, 2004. *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili.* Nairobi: Phoenix Publishers.

Halliday, M.A.K. 1970. *A Course in Spoken English: Intonation.* London: Oxford University Press.

Halliday, M.A.K. 1985. *An Introduction to Functional Grammar*. London: Edward Arnold Publishers.

Halliday, M.A.K. & J.R Martin. *2004. Introduction to Functional Grammar*: *3rd Ed.* Revised by Matthiessen M.I.M. London: Hodder Arnold.

Kibrik, A.E 1977. *The Methodology of Field Investigations in Linguistics.* Monton: The Hague – Paris.

Kihara, K.D. 2006. Uchambuzi wa Matini: Matumizi ya Lugha katika Sajili ya Matatu. M.A. Thesis. Kenyatta University. (Unpublished).

Kimble- Fry, A. 2001. *Perfect Pronunciation. A Guide for Trainers and Self-help Students.* Sydney: Clearspeak Pty Ltd.

Kioko, A.N. 2005. *Theoretical Issues in the Grammar of Kikamba – A*

*Bantu Language*. Lincom: EUROPA.

Ladd, D.R. 1996. *Intonational Phonology*. Cambridge: Cambridge University Press.

Levinson, S. C 1993. *Pragmatics*. Cambridge: Cambridge University Press.

Maw J. 1969. *Sentences in Swahili: A study of their Internal Relationships*. London: Luzac & Co. Ltd.

Malmkjær K. (ed.) 1991. *The Linguistics Encyclopedia*. London: Routledge.

Martinet, A. 1962. *Elements of General Linguistics*.London: Faber & Faber Ltd.

Matthews, P.H. 1981. *Syntax*. Cambridge: Cambridge University Press.

Mathooko, P.M 2004. Towards an Intergrative Perspective of Linguistic Accommodation: A case of Kikamba & Kitharaka. Ph.D. Thesis. Kenyatta University. (Unpublished).

Mohammed, M.A 2001. *Modern Swahili Grammar*. Nairobi E.A.E.P.

Munyao, M.K. 2006. The Morphosyntax of Kikamba Verb Derivations: A

Minimalist Approach. Tasnifu ya Uzamifu ambayo haijachapishwa. Chuo Kikuu cha Nairobi.

Mutiga, J.M 2002: The Tone System of Kikamba: A Case Study of Mwingi Dialect. Ph.D Thesis. University of Nairobi. (Unpublished).

Nkwera, F.M. 1978. *Sarufi na Fasihi: Sekondari na Vyuo.* Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.

Orodho, J.A. 2004. *Elements of Education & Social Science Research Methods*. Nairobi: Masola Publishers.

Pike, L.K. 1946. *The Intonation of American English*. Ann Arbor: University of Michigan Press.

Radford, A. 1997. *Syntactic Theory & structure of English*. Cambridge: Cambridge University Press.

Radford, A. 2004. *Minimalist Syntax. Exploring the Structure of English.* Cambridge: Cambridge Unviversity Press.

Richards, J, Platt J. & H. Weber. 1985. *Longman Dictionary of Applied Linguistics.* Hongkong: Longman Group Ltd.

Tallerman, M. 2005. *Understanding Syntax*: 2nd Ed. London: Hodder Arnold.

Trudgill, P. 1986. *Dialects in Contact*. Oxford: Basil Blackwell.

Williams, J.B. 1973. *Style & Grammar –A writers Handbook of Transformation*. New York: Dodd, Mead & Company.

William B. (ed.) Vol.2 1992. *International Encyclopedia of Linguistics*. Newyork: Oxford University Press.

## KIAMBATISHO

## SENTENSI SAHILI ZA KIKAMBA ZILIZOCHANGANULIWA

Sentensi hizi zimeainishwa kulingana na uamilifu: swalifu, arifu, amrifu, kanushi na mshangao.

**Sentensi Swalifu**

1. *Ala angĩ nĩmokĩte?*

   'Wale wengine wanakuja?'

2. *Mũsee kowĩnũkitye thĩna*?

   'Mzee kwani unapeleka shida nyumbani?'

3. *Nĩtĩũthi asala?*

   'Tutaenda hasara?'

4. *Syomĩtĩ aendie ĩndĩĩ?*

   'Syomiti alienda lini?'

5. *Mũinesa kwiw'a ũndũ ngwasya?*

   'Hamjasikia vile nasema?'

6. *Mũtũa akathi ũnĩ kwakya tene?*

   'Mutua ataenda kesho asubuhi na mapema?'

7. *Aendete Ilovi kĩ?*

   'Anaenda Nairobi kufanya nini?'

8. *Ũĩthyo wa ng'ombe nũyũ?*

'Chakula cha ng'ombe ndicho hiki?'

9. *Aũme nomaendaa kwa awe?*

'Wanaume hawaendi kwa waganga?'

10. *Tũnaĩ naku Wakyumwa?*

'Si tulikuwa na wewe Jumapili?'

**Sentensi Arifu**

1. *Aki nĩmanoaa mũno.*

'Waashi huchoka sana.'

2. *Ngũa ndune yĩ mĩisyo mingĩ.*

'Nguo nyekundu ina mikosi mingi.'

3. *Kĩkwũ kyake ti mana.*

'Kifo chake si bure.'

4. *Tangĩĩa thayũ waku.*

'Salimisha maisha yako.'

5. *Mbwaa sya maũũ nĩ ndaasa.*

'Kucha za miguu ni ndefu.'

6. *Kĩthima nĩ kyang'ala.*

'Kisima kimekauka'

7. *Ethwa nĩtũkumbũla, tũkaekewa.*

'Kama tutatubu, tutasamehewa.'

8. *Mwaitũ atũaa kũũ.*

'Mama huishi huku.'

9. *Anasomeaa Ilovi.*

'Alikuwa anasomea Nairobi.'

10. *Nawaie mũongo.*

'Ninaugua mgongo.'

11. *Kana kaũsũvĩlĩĩla ti kaseo.*

'Mtoto wa kubembeleza si mzuri.'

12. *Nĩngũvika mũsyĩ.*

'Nitafika nyumbani.'

13. *Nĩma yĩ mĩnoo mũno.*

'Ukulima unachosha sana.'

14. *Kwĩ mbevo mbingĩ mũno.*

'Kuna baridi nyingi mno.'

**Sentensi Amrifu.**

1. *Ete ĩkanda we!*

'Lete kamba wewe!'

2. *Vaa vaikalike athoosya angĩ!*

'*Hapa* pasiingie wachuuzi wengine!'

3. *Syana syonthe syĩende nza!*

'Watoto wote watoke nje!'

4. *Nĩenda ũvoya we!*

'Nataka kuomba wewe!'

**Sentensi Kanushi.**

1. *Ny'ie ndiũya.*

'Mimi sitakula.'

2. *Ny'e ndi ũndũ.*

'Mimi sina neno.'

3. *Satani nde syĩndũ sya mana.*

'Shetani hana vitu vya bure.'

4. *Ndũkone taweeka nesa!*

'Usione kama umefanya vizuri!'

5. *Ndwaĩle ĩkala mana!*

'Hupaswi kukaa bure.'

6. *Kũi wĩa!*

'Hakuna kazi!'

**Sentensi za Mshangao**

1. *Anake alũmu nĩmo aya!*

'Wavulana barubaru ndio hawa!'

2. *Kanga ti kaa!*

'Muhogo ndio huu!'

3. *Ula Ndukũ tyũũ!*

'Yule Nduku ni huyu!'

4. *Mũtindi akomie ĩmwe!*

'Mutindi alilala kabisa.'

5. *Mwa ndiĩla ũkwona tene!*

'Haki ni kitambo nilipokuona!'

6. *Kaĩ ũuaa nesa ũu*!

'Kumbe unapika vizuri hivi.'

KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY